KITENDAWILI

Mwaweza kuketi. Nimekuwa nikingojea muda mrefu kurudi huku Phoenix. Hakika nina furaha alasiri ya leo kuwa hapa. Ninapokuwa Phoenix, kuna jambo fulani kuihusu, daima hunifanya nijisikie ya kwamba nimeketi miongoni mwa watu ambao ni rafiki zangu, ambao wananipenda. Na—na ni mashujaa wakuu wa maombi walitoka hapa kuniombea, kwa miaka kadhaa. Daima mimi hukumbuka ule mkutano wa kwanza niliokuwa nao hapa pamoja na Ndugu Outlaw, Ndugu Garcia, na wahudumu hapa wa mjini. Jinsi ambavyo Bwana alibariki nilipokuwa tu katika ujana wa mikutano yangu! Tangu wakati huo, Phoenix imeshikilia ninii kuu. . . Jambo fulani liko moyoni mwangu, ambalo ni gumu kuelezea.

2 Kama mvulana mdogo, daima nilitaka kuja Phoenix. Sikuzote nilisoma kuhusu jangwa. Nilikuwa na mashairi madogo niliyotunga kuuhusu, nilipokuwa tu mvulana mdogo, kuhusu Arizona.

3 Nina furaha sana kuwa mwe—mwenyeji sasa. Nadhani nina kama mwaka mmoja tu, na labda zaidi kidogo. Bali hupati wengi sana walio na umri mkubwa kuliko huo. Kila mtu ninayekutana naye, nasema, "Je! wewe ni mwenyeji?"

"Vema, kadiri kulivyo nao. Nimekuwa hapa kwa muda."

4 Na—nami nadhani inanibidi kupanda kwenda kwenye ardhi iliyohifadhiwa ya Apache, ama mahali fulani, kumpata mwenyeji halisi.

5 Ndipo mtu fulani alisema, sio muda mrefu uliopita, kasema, "Ndugu Branham, unaonaje Arizona?"

6 Nikasema, "Vema, imekuwa ni moja ya matarajio yangu makubwa ya maishani, ku—kuishi Arizona, Naye Mungu amenijalia hilo."

7 Tuko hapa kabla tu ya mkutano wa Wafanya Biashara, ambao umekuwa ni kitu cha kila mwaka kwetu. Na alasiri ya leo, tunapokusanyika hapa kwa ajili ya mkutano wa kutangulia kabla ya mkutano huo ambao unaanza Alhamisi usiku, ninaamini. Imekuwa ni majaliwa yangu, kwa miaka michache i—iliyopita, kuja na kufanya mikutano hii midogo huku, kabla ya mkutano halisi kuanza kwenye. . . ama mkutano mkuu, hasa, kuanza.

8 Naye Ndugu Williams ni rafiki mpendwa sana, yeye pamoja na Dada Williams. Hakika ninawapenda sana watu hao kwa moyo wangu. Sikuzote wananialika nirudi, na kwa hiyo tuna furaha kutimiza mwaliko huo alasiri ya leo.

9 Pia humu jukwaani, Ndugu Fuller, Ndugu Jewel Rose, na Ndugu Tony Stromei kutoka Tucson, na Ndugu Borders meneja wetu wa uamsho. Na ndugu m—mzuri wa thamani, Arganbright, tumekuwa pamoja katika vita vingi vikali. Kwenye ng'ambo ya pili ya mto; ninatarajia kuishi pamoja naye kwenye ng'ambo ya pili ya ule mto mkuu siku moja.

10 Siwezi kulikumbuka jina la ndugu huyu, nimejaribu. Jina lako ni nani, ndugu? [Ndugu anasema, "Al Booher."—Mh.] Booher, Ndugu Booher. Na—najua uso wake. Na hivi wewe siye wakati mwingine anayewafasiria . . . ["Kuwafasiria viziwi."] viziwi. Hiyo ni . . .

Nasi tuna furaha sana kuwa nanyi nyote hapa.

11 Nilikuwa tu nikiangalia hapa chini mbele yangu, nami ninaona baadhi ya rafiki zangu kote kote kutoka Arkansas, hapa. Nilipokuwa hapa kwa mara ya kwanza, niliwaambia ya kwamba kila nilikoenda, nilipata mtu kutoka Arkansas. Nina hakika, kama nikifika Mbinguni, nitakutana na wengine kule kutoka Arkansas, maana hakika wamekuwa ni watu waaminifu, watiifu.

12 Na sasa, kwa kawaida mimi huzungumza muda mrefu, bali nimejaribu niwezavyo kwa namna fulani kuandaa Maandiko yangu na muhtasari kusudi nisizungumze muda mrefu kupita kiasi. Pia ninataka kuwaombea wagonjwa wakati nikiwa Phoenix.

13 Sasa, Ujumbe ambao mimi . . . Bwana amenipa, wakati mwingine, mwajua, mambo haya yanakera sana. Na imekuwa hivyo katika kila wakati. Nami nimejaribu niwezavyo kudumu pamoja Nao. Ni jambo fulani. Na kama sikusema jambo lile ambalo Mungu aliniambia, na kama ilikuwa—isingekuwa ni la Mungu, basi Yeye . . . lisingekuwa kwenye Neno. Lakini kama liko kwenye Neno, na ahadi kwa ajili ya wakati huu, basi ninajisikia ya kwamba ninafanya yaliyo haki, kwa kuwa ninajaribu tu kudumisha kile alichoahidi kwa ajili ya saa hii.

14 Na mara nyingi wakati usipokubaliana na mtu katika theolojia yao, mtakosana nao, upesi sana. Bali hilo halipaswi kutokea. Ninajaribu kuninii . . . Ninapata marafiki zangu walio wa madhehebu mbalimbali ya makanisa, na kadhalika, sikosani na hao ndugu. Jamani, ninaenda makanisani mwao, kila mahali wanaponiruhusu kuja, na kuhubiri. Bali haitupasi kukosana, juu ya mawazo madogo.

15 Lakini, mwajua, kama nilisema jambo lolote tofauti na yale yaliyo moyoni mwangu, ningekuwa mnafiki. Nami ni—ni . . . Na iwe mbali nami! Huenda ikanibidi kukutana Naye siku moja, kama mwenye dhambi, bali kwa hakika sitaki kukutana Naye kama mnafiki. Bali nataka kuwa mkweli. Na kama tu ningalisema, "Vema, nitaliacha tu Hili kwa kuwa hao wengine wanaamini *hili*, *lile*," basi ni mtu wa aina gani? Msingeweza

kuwa na imani kwangu, nami nisingekuwa na imani kwa Mungu wala kwa nafsi yangu, wakati nikipatana kwa urahisi jinsi hiyo.

16 Mtu yeyote hana budi kuwa na jambo fulani walilo na hakika nalo. Na hapo ndipo unapoweza kuitilia imani yako msingi, ni wakati ukiwa na hakika. Lakini mpaka utakapokuwa na hakika, kukiwepo na swali, liache mpaka utakapokuwa na hakika.

17 Sasa Billy labda amesambaza kadi za maombi, ambazo ninafikiri ameninii . . . Naam, nilimwambia azisambaze. Nami ninaamini aliniambia, muda mfupi uliopita, ya kwamba amezisambaza. Mahali fulani pale, nitawaita wachache kwenye mstari wa maombi, baada ya kitambo kidogo, wapate kuombewa. Na iwapo kadi yako haijaitwa . . . Kama—kama ikiitwa, hasa, nawe huna hakika kwamba Mungu Ndiye mponyaji na atakuponya, haitafaa kitu kuja huku juu, kwa maana hutaponywa. Wewe, iwapo pana swali moja, unasema, "Vema, sasa, kama kuna jambo fulani maishani mwangu, hakika inanipasa kulinyosha hili," nenda kalinyoshe hilo, kwanza, kisha urudi kwenye mstari wa maombi, unaona.

18 Kwa sababu, uponyaji ni mkate wa watoto. Tunatambua hilo. Uko katika upatanisho, na upatanisho unatumika mioyoni mwetu kwanza. Nao uponyaji sikuzote umeutangulia kila ujumbe, na pia umekuwa ni njia ya kuwakusanya watu pamoja. Na ni ninii . . .

19 Watu wengi wataudhamini mkutano wa uponyaji, wengi watahudhuria mkutano wa uponyaji, ama sherehe za nyimbo, bali inapofikia kuokolewa kwa maskini nafsi iliyopotea, hakuna watu wengi wanaovutiwa na hilo. Wananinii tu . . . Lakini hilo ndilo jambo muhimu. Uponyaji wa Kiungu na sherehe za nyimbo, na kadhalika, ni ninii tu . . . Kama vile Ndugu Bosworth alivyozoea kusema, "Ni chambo kwenye ndoana." Nawe unamwonyesha samaki chambo, sio ndoana.

20 Na jambo ndilo hilo tu, kuwafanya watu wasikilize kwa kitambo kidogo, mpaka unapoweza kuwapa ujumbe wako. Mungu amefanya hilo kwa kila wakati, kupitia kila wakati, daima kumekuweko na uamsho wa uponyaji. Na kama ni uamsho halisi wa uponyaji, nyuma ya uamsho huo, daima, kuna ujumbe. Kamwe ishara haitolewi kwa ajili ya ishara tu; inautangulia ujumbe fulani.

21 Nami ninaamini ni jambo lile lile, miaka kumi na saba iliyopita, ama miaka kumi na minane sasa, ambapo Bwana alinituma nikaanze kuwaombea wagonjwa. Ilisababisha uamsho mkubwa miongoni mwa watu. Watumishi wengi mashuhuri wa Mungu wamejitokeza na miamsho ya uponyaji, na, ila uamsho wa uponyaji, wenyewe, kama wewe ungali unakaa kwenye mwendeleo ule ule wa kale wa kile umekuwa sikuzote, kuna kasoro, uamsho huo wa uponyaji haukutumwa kutoka kwa

Mungu. Hauna budi kuuvutia usikivu kwanza, mnaona, kuvutia usikivu, ndipo ujumbe unatolewa.

22 Yesu, wakati alipotokea, akiwaponya wagonjwa, na kadhalika, Yeye alikuwa ni Nabii mkuu kwa hao wote. Bali alipoanza kuwaambia Kweli, ya Injili, kwamba Yeye alikuwa ni Nani na sababu ya kuja Kwake, basi alikuwa—hakupendwa na watu baada ya hapo. Na hivyo ndivyo imekuwa daima kote katika kila wakati, na itaendelea vivyo hivyo.

23 Sasa tupo hapa alasiri ya leo, halafu kesho alasiri katika chumba kiki hiki. Yote ni kwenye saa moja. Hiyo ni kweli, ndugu? [Ndugu anasema, "Saa moja na nusu."—Mh.] Saa moja na nusu, kesho alasiri, ama jioni, halafu Jumanne jioni. Nami nafikiri Jumatano jioni, pia. ["La, kwenye Hoteli ya Ramada, Jumatano."] Kwenye Hoteli ya Ramada, Jumatano. Halafu Alhamisi basi, hiyo ni kweli, m—mkutano unaanza. Na Bwana akipenda, ninataka kuihudhuria hiyo yote.

24 Nipo hapa, ndugu yenu, msaidizi katika Ufalme wa Mungu, kuwasaidia kwenye chochote niwezacho. Kujibu swali lako, huenda nisiweze kulijibu. Bali, kwa maombi, labda tungefahamu kama tungeliombea na kumwendea Mungu kulihusu, pasipo kutoa maoni yetu wenyewe.

25 Kama wewe ni mgonjwa, laiti ningaliweza kukuponya, ila hamna mtu anayeweza kufanya hivyo. Umefanyika tayari. Uponyaji unakaa ndani yako. Ni imani yako katika kazi ambazo Mungu alifanya Kalvari, pamoja na Yesu Kristo. Na nje ya hapo, hamna uponyaji; na nje ya hapo, hamna wokovu; hamna kanisa, hamna dhehebu, hamna matambiko, hamna kitu kilicho na wokovu. Yesu Kristo, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa. *Alijeruhiwa* kwa makosa yetu, makosa," samahani, "kwa kupigwa Kwake sisi *tuliponywa*," yote ni katika wakati uliopita, "tuliponywa." Sasa, juu ya hilo!

26 Sina ila dakika chache tu za kuzungumza, alasiri ya leo, kuwazungumzia, labda dakika ishirini, thelathini, halafu tutafanyiza mstari wa maombi. Kila siku, kama kawaida, watu wapya wanaingia, kwa hiyo kutakuwako na kadi mpya za maombi zitakazosambazwa. Bali tutafanya yote tuwezayo, yote ambayo Mungu ataturuhusu kufanya, kumwombea kila mgonjwa anayekuja, anayetaka kuombewa.

27 Kama kuna kitu kama mtu anayekuja kwa ndege, anayekufa, hali ya dharura ama kitu fulani, mbona, waweza kumwona Ndugu Williams, Billy Paul, ama baadhi yao kuwaingiza chumbani, kwamba hawataki kuninii. . . Hawawezi kuketi, wanakufa, hawana budi kuhudumiwa sasa hivi, vema, wawekeni kwenye chumba kimoja nipate kuwaendea mara moja.

28 Lakini ni bora zaidi, kama huko kwenye hali hiyo ya dharura, kwamba wewe—kwamba wewe utachukua tu kanuni zako za imani na—na imani zako, na kuzisukumia kando

tu dakika chache, muda mrefu kutosha tu kusikiliza yale Maandiko yasemayo, na halafu yale Mungu afanyayo kuhusu yale aliyoahidi. Na hilo litajenga imani. Na hata hutahitaji kuwa kwenye mstari wa maombi, wala mtu yeyote kukuombea. Umeponywa tayari, kama tu unaweza kuamini hilo. Unaona? Na hilo ndilo kusudi lake, ni kukuwezesha, ni kukufahamisha, wewe, yale ambayo Yesu amekufanyia.

29 Si lazima uje hapa juu na kupiga magoti, na kuomba kwa bidii, mpaka—mpaka umeokoka. Umeokoka tayari, bali inakupasa kukubali. Maombi yako hayatoshi. Imani yako ndiyo inayokuokoa, si kwa maombi. Lakini, "Kwa imani mmeokolewa." Jambo lile lile kwa uponyaji. Nina hakika sisi sote tunafahamu hilo.

30 Na iwapo kuna wageni malangoni petu, tunataka mjue ya kwamba, kwangu mimi, ama kundi hili nililo nalo hapa, Wafanya Biashara wa Full Gospel, hatuwakilishi dhehebu lolote. Tunawakilisha tu waaminio Wakristo katika madhehebu yote. Kila mtu amekaribishwa. Tunafurahia tu kuwa nanyi. Unasema, "Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa fulani, je! ningeweza kuombewa?" Hata haikubidi kuwa mfuasi wa kanisa, haikubidi kufanya lolote ila kuja hapa juu na kumwamini Mungu. Hilo tu ndilo unalopaswa kufanya. Mungu hufanya hayo mengine.

31 Sasa, mimi—mimi...nimeichakaza Biblia moja, tangu nilipoanza katika miamsho ya uponyaji, ama kuwaombea wagonjwa, hasa. Huko Houston, Texas, nilipewa Biblia, miaka kadhaa iliyopita, miaka kumi na minane iliyopita, na Ndugu Kidson na kundi lake. Nami nikaichakaza Biblia hiyo, huku na huku, kote ulimwenguni, mpaka ikachakaa kabisa, kurasa zikatoka.

32 Ndio kwanza tu nipewe Biblia mpya. Na ajabu ni kwamba...Mimi si mshirikina; natumaini ninyi watu hamnidhanii kuwa mshirikina. Wakati nilipopewa Biblia hii, walikuwa na ninii ndogo... vitia alama viwili vidogo mle, riboni ndogo. Ni Biblia kama niliyokuwa nayo.

33 Ndugu Kidson alinipa moja iliyokuwa ni Biblia ya Scofield, sasa, sio kwa sababu ninakubaliana na Bw. Scofield katika muhtasari wake. Sasa, labda baadhi yenu mnakubaliana nayo, wengine wenu hamkubaliani, bali ninawataka mjue ya kwamba kamwe siichukui Biblia ya Scofield kwa kuwa ninaamini hayo. Kwa sababu, yeye ameigawa vizuri katika aya hata ninaninii... Hiyo ilikuwa moja ya Biblia zangu za kwanza, nami nilijifunza tu kuisoma namna hiyo. Nami ninaiweka tu Biblia hiyo hiyo. Ambayo, kama ningalikuwa na ile ya Mfululizo ya Thompson, ingalikuwa ni nzuri zaidi. Ningaliweza kupata vifungu vyangu upesi zaidi kwenye ile ya Mfululizo wa Marejeo ya Thompson.

34 Lakini nilipoifungua Biblia, utepe wa kwanza katika Biblia hiyo ulikuwa ni kitu cha ajabu sana, mahali ilipokuwa. Ulikuwa

ni wakati Sulemani alipoliweka wakfu hekalu la Mungu, nao Utukufu wa Mungu ulikuwa ni mkuu sana, utukufu wa Shekina kwenye jengo hilo, hata makuhani wasingeweza kuhudumu.

35 Halafu uzi wa pili ulikuwa mahali ambapo Ezra alirudi na kuliweka hekalu wakfu.

36 Kisha kitia alama kidogo cha tatu, ambacho mke wangu alikuwa amenipa na kukiweka katika Biblia, bila kujua, kikiwa na jina langu, na kadhalika, kilikuwa kwenye Marko 11:22. Alikiingiza tu kwenye Biblia, na hapo ndipo kilipokuwa, kwamba, "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka.'" Nanyi nyote mnajua wakati Andiko hilo lilipokuwa moyoni mwangu, ninyi watu wa kanda, hapo ndipo wale kuchakulo walipokuja moja kwa moja, wakaingia kwenye—kwenye . . . .Hiyo ni kweli kabisa.

37 Halafu jambo la ajabu ni kwamba, yule ndege ninayempenda sana, robini, picha yake ilikuwa kwenye kitia alama hicho, maskini yule ndege mdogo mwenye kifua chekundu. Kama vile ile hekaya kuu isemavyo, kwamba wakati mmoja alikuwa ndege wa hudhurungi; bali kulikuwako na Mtu aliyekuwa akifa, siku moja, msalabani, naye akamhurumia Mtu huyo sana hata akaruka akaja kujaribu kuing'oa misumari hiyo yeye mwenyewe, naye akalowa damu kifuani mwake mwote, na tangu wakati huo amekuwa na kifua chekundu. Hivyo ndivyo ni—ninavyotaka kumlaki Mwokozi wangu, pia, nikiwa na Damu Yake kwenye ninii yangu . . . ndani ya kifua changu, moyoni mwangu.

38 Halafu mkutano wangu wa kwanza, Ujumbe ninaopaswa kuhubiri hapa, uko huko Phoenix, Arizona. *Phoenix* ni kitu kinachoweza kuinuka mahali patupu. Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo. Yeye huchukua kitu bure, anainua kitu fulani kutoka kwake.

39 Nao Ujumbe wangu alasiri ya leo, unaitwa, kwa dakika thelathini ama arobaini zifuatazo, "kitendawili." Nami ninataka kusoma kutoka kwenye Maandiko ambayo . . .

40 Miaka michache iliyopita, ambapo, ningeitwaa Biblia, na niache unipe Biblia, wakati nilipoanza huduma yangu; na unachukua tu Biblia yako, na wengi wenu mmeniona nikifanya hivyo, ninaifungua tu namna *hiyo*, na kusema, "Bwana, U wapi Ujumbe wangu?" Ilifunguka kwenye Yoshua, mlango wa kwanza, Biblia yoyote ungaliweza kunikabidhi.

41 Mpaka usiku mmoja ono likatokea, ambalo mnalifahamu, nami nikaiona Biblia hiyo ikishuka toka Mbinguni, na mkono wenye ukosi kwenye sijafu, namna *hii* ukashuka chini kwenye vifungu tisa vya kwanza vya Yoshua.

42 Hapo ndipo ninaposoma, alasiri ya leo, kwa somo langu, ama somo langu la Maandiko. Somo langu linapatikana kwenye kifungu cha 10 na ninii—ninii . . . Ninamaanisha mlango wa 10 na kifungu cha 12.

43 Kabla hatujaifungua Biblia, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja. Sasa huku vichwa vyetu na mioyo yetu imeinamishwa, hebu na tuwazie hili. Hebu huu usiwe tu ni mkutano wa kawaida; tunayo hiyo wakati wote. Lakini hebu na tumwombe Mungu, kila mmoja wetu, kwamba huu uwe usio wa kawaida sana, hivi kwamba Uwepo wa Mungu utaendelea kuwa pamoja nasi kote mkutanoni.

44 Baba wa Mbinguni, tunashukuru kwa ajili ya majaliwa haya mazuri sana na ya kupendeza kuwa hapa Phoenix alasiri ya leo, tumekusanyika katika chumba hiki kikuu cha mikutano hapa, miongoni mwa watu hawa. Na sasa sisi tuko tu karibu kulikaribia Neno. "Nalo Neno lilifanyika mwili likakaa kwetu." Na jalia iwe tena, Bwana, kwamba Neno litafanyika mwili, litamiminika katika kanisa Lako na watu Wako, lipate kutimiza ahadi za wakati huu.

45 Tunapotambua kwamba tuna—tunaumalizia wakati, wakati unaisha. Unachanganyikana na Umilele. Nasi tuko kwenye Pwani ya Magharibi. Na kama vile ustaarabu umesafiri, Mashariki hata Magharibi, vivyo hivyo Injili imesafiri pamoja nayo. Na sasa hamna mahali pa kwenda ila ni kurudi Mashariki tena. Umekamilika.

46 Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba hii itakuwa ni saa kuu kwa ajili yetu sisi sote, kwamba tuuhisi Uwepo wa Roho Mtakatifu, Mwandishi wa Neno hili, katika jengo la maskani ya mwili tena; akijidhihirisha Mwenyewe kwetu, katika kuzisamehe dhambi zetu, kusamehe uovu wetu, pamoja na hakikisho ya kwamba hatamhesabia mwaminio dhambi, pamoja na hakikisho la hiyo. Na pia kwamba atayaponya magonjwa yetu, na kuwaondoa wa—watu kutoka kwenye viti vya magurudumu na kutoka kwenye mikongojo; na kuwapa kuona, hao walio vipofu; na—na nyongeza ya siku, kwa hao wanaokufa kwa magonjwa mabaya sana kama kansa na kifua kikuu, mabaya, na magonjwa ambayo madaktari wetu hawawezi kuyazuia. Yamewashinda, bali, Mungu, Wewe unapita utafiti wote wa kisayansi. Unapita hoja zote. Wajalie watumishi Wako, alasiri ya leo, kunena na kulisikia Neno Lako, juu ya somo: *Kitendawili*. Kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

47 Sasa katika Biblia, Yoshua mlango wa kwanza, na Yoshua mlango wa 10. Mlango wa kwanza na kifungu cha kwanza.

> *Ikawa baada ya kufa kwake Musa, mtumishi wa* BWANA, BWANA *akamwambia Yoshua, mwana wa Nuni, mtumishi wa Musa, akasema,*

> *Musa mtumishi wangu amekufa; haya basi, ondoka, vuka mto huu wa Yordani, wewe na watu hawa wote, mkaende hata nchi niwapayo wana wa Israeli.*

Kila mahali zitakapopakanyaga nyayo za miguu yenu, nimewapa ninyi, kama nilivyomwapia Musa.

Tangu jangwa hili na mlima huu, Lebanoni, mpaka mto ule mkubwa, mto wa Frati, nchi yote ya Wahiti, tena mpaka. . . upande wa machweo ya jua, hapo ndipo patakapokuwa mpaka wenu.

Hapatakuwa mtu yeyote atakayeweza kusimama mbele yako siku zote za maisha yako; kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe; sitakupungukia wala sitakuacha.

Uwe hodari na moyo wa ushujaa, maana ni wewe utakayewarithisha watu hawa nchi hii niliyowaapia baba zao ya kwamba nitawapa.

Uwe hodari tu na ushujaa mwingi, uangalie kutenda sawasawa na sheria yote aliyokuamuru nanii wangu. . . *aliyokuamuru Musa mtumishi wangu; usiiache, kwenda mkono wa kuume, au wa kushoto, upate kufanikiwa sana* kila *uendako.*

Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa humo; maana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana.

Je! Si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa B*WANA*, *Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendako.*

48 [Ndugu Branham sasa anasoma Yoshua 10:12-14—Mh.]

Ndipo Yoshua akanena na B*WANA katika siku hiyo ambayo* B*WANA aliwatoa Waamori mbele ya wana wa Israeli; akasema mbele ya macho ya Israeli,* Simama kimya juu. . . *Wewe Jua, simama. . . kimya juu ya Gibeoni; na wewe Mwezi, simama katika bonde la Aiyaloni.*

Ndipo jua likasimama kimya, na mwezi ukatulia, hata hilo taifa lilipokuwa limekwisha jipatiliza juu ya adui zao. Hayo je! Hayakuandikwa ndani ya kitabu cha Yashari? Basi jua likasimama kimya katikati ya mbingu, wala halikufanya haraka *kuchwa kwa muda wa siku nzima.*

Haikuwapo siku nyingine mfano wa siku hiyo katika siku zilizotangulia mbele yake wala katika hizo zilizoandama baada yake, hata ikawa yeye B*WANA kuisikia sauti ya binadamu; kwa kuwa* B*WANA alipiga vita kwa ajili ya Israeli.*

49 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Maneno Yake. Sasa somo alasiri hii: *Kitendawili*.

50 Sasa, neno *kitendawili*, kama vile nimekuwa nikilichunguza na kuhakikisha kwamba—kwamba nililipata, neno *kitendawili* linamaanisha, kulingana na Webster, kwamba ni "jambo lisilosadikika, bali ni kweli." Sasa, mwajua, tumesikia ule msemo wa kale, kwamba—kwamba, "Ukweli unaninii zaidi" (wanausemaje huo?) "ni wa kigeni zaidi kuliko hekaya," ndivyo ukweli ulivyo. Kwa kuwa, mtu anaposema ukweli, wakati mwingine ni wa kigeni sana.

51 Ninamjua rafiki yangu mmoja, ambaye, huko Kolorado. Walikuwa wanaendeleza hesabu, walitaka kuwahesabu kulungu. Basi kulikuwa na kulungu ishirini na mmoja kwenye kundi. Naye rafiki yangu, wakati, alikuwa amerudi huko kuwinda, wakati waangalizi walipokuja. Nao walikuwa wamelipa gharama kubwa, hifadhi ilikuwa imeilipia, kwa moja ya magari haya ya barafu, warudi wakawahesabu kulungu. Akasema, "Haikuwapasa kutumia fedha hizo zote. Ninaweza kuwaambia kuna kulungu wangapi huko nyuma." Nao wakamcheka tu. Kasema, "Ni wangapi?"

52 Akasema, "Wako kumi na tisa." Kasema, "Kulikuwako na ishirini na mmoja, nami nikawaua wawili."

53 Naye mwangalizi akamcheka. Umeruhusiwa tu kumwua mmoja, mwajua. Naye akasema, akasema, "Naam, ninajua uliwaua."

54 "Vema," kasema, "hivyo ndivyo nilivyofanya. Kulikuwako na kulungu ishirini na mmoja, nami nikawaua wawili."

55 Basi huyo msimamizi akacheka tu na kurudi. Na hao ndio waliokuwako, kulungu kumi na tisa. Mnaona?

56 Akanigeukia, akasema, "Unaona, mchungaji, sema tu ukweli, watu hawatasadiki." Mnaona, sema tu ukweli, kwa hiyo hakika ni wa kigeni kuliko hekaya.

57 Yoshua hapa ni Kitabu, kweli, ni Kitabu cha ukombozi, cha Agano la Kale. Yoshua, ingetupasa kukihesabu kuwa hivyo, Kitabu cha ukombozi. Kwa kuwa, ni, ukombozi una sehemu mbili. Ukombozi, mahali popote, una sehemu mbili. Hizo ni, ni "kutoka" na "kuingia." Inahitaji sehemu mbili kufanya ukombozi, "kutoka," "kuingia."

58 Musa aliiwakilisha torati iliyowatoa Misri, na, ambapo, Yoshua aliwakilisha neema iliyowapeleka kwenye nchi ya ahadi. Vinginevyo, ilikuwa, to—torati na neema zilikuwa ni sehemu mbili tofauti za amri ya Mungu. Sasa, torati iliwatoa, Musa, naye Yoshua akawaingiza.

59 Pia inawakilisha kitu fulani kwa ajili ya siku yetu. Sasa inawakilisha, walivyokuwa safarini, wakitoka—wakitoka Misri kuingia kwenye nchi ya ahadi, vivyo hivyo nasi tumetoka ulimwengu wa Misri, machafuko, tukielekea kwenye Nchi ya ahadi. "Nyumbani mwa Baba Yangu kuna makao mengi; kama

sivyo, ningaliwaambia," Yohana 14. Kutoka "nje ya," kuingia "ndani ya."

60 Torati ndiyo inayotufanya tujue tumekosea, bali neema ndiyo inayotusamehe. Torati haina matumaini ya—ya ukombozi, kwa sababu . . . na kuikamilisha. Haina neema, kwa maana torati inaonyesha tu kwamba wewe ni mwenye dhambi, bali neema inakwambia jinsi ya kutoka humo. Torati ni polisi anayekuweka gerezani, bali ukombozi Ndiye Yule aliyekuja na kuilipia faini yako; na "kutoka," na "kuingia," kuingia kwenye neema.

61 Waefeso. Sasa tunaona jambo lile lile, Agano la Kale, nafikiri Kitabu hiki cha Yoshua kinafaa. Neno linalokifaa, lingekuwa, Kitabu cha Waefeso cha Agano la Kale. Kitabu cha Waefeso cha Agano la Kale, lingekuwa ni jina zuri la kukiita Kitabu hiki cha Yoshua, kwa maana hakika linastahiki kwa hiki.

62 Sasa tunaona Yoshua akiwakilisha neema, ama upatanisho, kwamba haingekuwepo kwenye wakati ule ule torati ilipokuwepo.

63 Wala ujumbe wowote, unaowapeleka watu mbele, kamwe haupatani na ujumbe uliopita. Hautapatana. Hapo ndipo mlipo na shida leo hii. Yesu alisema, "Hivi mtu yeyote huchukua ki—kiraka kipya cha nguo na kukitia kwenye vazi kuukuu? Ama kuweka divai mpya kwenye viriba vikuukuu? Huharibika. Huvipasua." Haviwezi kuistahimili.

64 Wala Yoshua kamwe asingaliingia kwenye huduma yake mpaka baada ya Musa kuondoka. Kwa hiyo unaona kifungu cha kwanza kabisa hapa, "Musa mtumishi Wangu amekufa; sasa ondoka ukawapeleke watu hawa kwenye nchi ya ahadi." Musa, akiiwakilisha torati, ilikuwa imeutumikia wakati wake. Ni, torati ilikuwa imetumikia wakati wake.

65 Walianza safari, kweli, kwa neema, kwanza. Kabla ya kuwa na torati, walikuwa na neema. Wakati wakiwa Misri, pasipo na torati; hakukuwako na mtu huko chini, ni makuhani tu, na kadhalika, bali hawakuwa na torati yoyote. Torati haikuwa imetolewa bado. Neema iliwapa nabii. Na, pia, neema ilileta upatanisho, mwana-kondoo wa sadaka. Tutaingilia jambo hilo juma hili, juu ya sadaka, damu, kwa maana hapo ndipo penye uponyaji wenu. Kwa hiyo juu ya ninii . . . Upatanisho ulikuwa umetolewa kabla hapajakuwapo na torati yoyote. Neema ilikuwepo kabla ya torati, wakati wa torati, na baada ya torati.

66 Kwa hiyo huyo hapo Yoshua, akiiwakilisha neema, alikuwepo moja kwa moja pamoja na torati, bali isingeweza kutumika mradi tu torati iko mahali pake hasa.

67 Na vivyo hivyo ulimwengu wa kanisa katika siku hizi za mwisho! Umekuja, umetumika mahali pake, bali wakati unakuja ambapo hauna budi kwisha. Hauna budi kwisha. Hapana budi kuwepo na Waefeso, pia, ya safari hii, kama tu

kulivyokuwa na ya safari zingine. Waefeso haina budi kuja, Waefeso, Waefeso ya safari hii. Angalieni.

68 Ambapo hiyo torati isingeweza kumwokoa mwenye dhambi, kama nilivyoelezea. Isingeweza. Kwa hiyo ile nchi ya ahadi iliwakilisha siku ya neema. Mnaona, asingeweza kuwaingiza ndani, katika safari hiyo.

69 Na kama mliona, katika safari hiyo, walikuwa na hatua tatu za safari yao. Kwanza ilikuwa ni maandalizi kwa imani, huko Misri, chini ya mwana-kondoo wa sadaka. Kisha wakaivuka Bahari ya Shamu, wakaingia nyi—nyikani, utengano, ambao uliwakilisha hatua nyingine ya safari hiyo.

70 Maana, chini ya maandalizi, wakati wote walipokuwa tayari, basi walipofika kwenye—kwenye Bahari ya Shamu, palikuwapo na kushindwa tena. Hao watu hawakuamini, baada ya kuona mambo mengi ambayo Mungu alikuwa amefanya. Wangali hawakuamini. Ndipo Mungu akaifungua Bahari ya Shamu na kuwapeleka, ambapo tunafundishwa ya kwamba watu wote walibatizwa wawe wa Musa, chini ya Wingu na katika bahari.

71 Sasa walibatizwa, walitubu na kubatizwa, kisha wakaja kutembea katika maisha mapya, katika nchi mpya, katika upya wa safari, miongoni mwa watu wapya, huku mkono wa Mungu ukiwa juu yao. Bali hatimaye ilifika mahali, katika safari hii waliyokuwa nayo, ambapo hawakuridhika na mwendo wao wa neema. Iliwabidi kulifikia jambo fulani ambalo wangelifanya wenyewe.

72 Sasa hapo ndipo watu wanapowazia, leo hii, juu ya uponyaji wa Kiungu, ama kazi nyingine yoyote ya neema, ya Mungu, kwamba kuna jambo unalopaswa kufanya. Wewe, hakuna lolote unalopaswa kufanya ila kuamini, mwamini tu Mungu.

73 Na, hao, laiti wangaliendelea! Hawakupewa ahadi hiyo chini ya torati. Ahadi ilitolewa kabla ya torati, pasipo na masharti yoyote kwake, "Nimewapa nchi hii, nendeni kule!" Lakini kabla hawajaifikia ahadi hiyo, waliamua kuna jambo wanalopaswa kufanya wenyewe.

74 Na, hilo, tungali tunapata hilo miongoni mwa wanadamu. Tuna mwelekeo wa kuwa jinsi hiyo, "Kuna jambo tunalopaswa kufanya." Tunajisikia hivyo, kwamba tuna sehemu mle pia.

75 Kweli una sehemu mle, hiyo ni kuyasalimisha mapenzi yako, mawazo yako, kwa mapenzi na wazo la Mwenyezi Mungu, na imekwisha. Hakuna lingine. Ichukue tu ahadi Yake, usiwazie lingine. Tembea nalo, ndipo Mungu anafanya hayo mengine.

76 Kisha walitaka torati. Naye Mungu daima hukupa shauku ya moyo wako; Yeye aliahidi kufanya hivyo. Ila tunaona, walipopiga hatua moja kutoka kwenye upande wa yale Mungu aliyowaahidi awali, basi huo ulikuwa mwiba katika mwili mpaka torati

ilipoondolewa, mpaka Yesu Kristo alipokuja na kusulibishwa kuiondoa torati. Ilikuwa ni mwiba katika mwili.

77 Na chochote unachojaribu kufanya kwa nafsi yako, daima kitakuletea aibu. Kitakuletea matokeo mabaya. Mwamini tu Mungu, na hilo latosha. Kile Mungu alichoahidi, "Mimi ni Bwana Mungu Wako niyaponyaye magonjwa yako yote." Unaona? "Akitokea mtu kati yenu, mgonjwa, na awaite wazee wa kanisa." Yeye aliahidi, "Kazi alizofanya Yeye, zingefanywa kanisani Mwake."

78 Ni kwa nini inatubidi kuyakubali madhehebu, na kadhalika, ambayo yatafutilia hayo mbali kutoka kwenye Kitabu? Mnaona, i—inakuwa ni mwiba katika mwili. Na hapa kwenye wakati wa mwisho, tunakabiliana na jambo hilo tena, uso kwa uso, ni juu ya Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, na wowote wale, mnaona. Wewe, huwezi kuendelea; huna budi kurudi kwenye Injili nzima yote. Ilifanywa kwa ajili ya mtu mkamilifu, na Mungu mkamilifu aliyefanyika mwili na kukaa miongoni mwetu. Nasi tunajua ya kwamba mambo hayo ni kweli.

79 Sasa kama tukiangalia, basi, safari yao nyikani ndipo walipofanya kosa lao lililo kuu mno ambalo Israeli ilipata kufanya, mpaka Kalvari, lilikuwa wakati (katika Kutoka 19) waliikubali torati badala ya neema. Walikuwa na neema. Walikuwa na nabii. Walikuwa—walikuwa na mwana-kondoo wa sadaka. Walikuwa na ukombozi. Walikuwa wamepitishwa kwenye Bahari ya Shamu. Walikuwa wameponywa magonjwa yao. Walipata maji kutoka kwenye mwamba uliopigwa. Walikuwa—walikuwa na mana kutoka mbinguni. Kila walichohitaji walikuwa wamepewa, nao wangali walitaka kitu kingine.

80 Sasa huo ni mfano mkamilifu wa Waefeso yetu siku hizi, kweli kabisa. Tulitoka chini ya Luther; tukapitia kwenye utakaso, chini ya Methodisti; na kuingia kwenye kurudishwa, chini ya Pentekoste. Jinsi hasa ilivyokuwa, ile safari ya nyikani. Ndipo Mungu alipotutoa, tulifanikiwa sana. Lakini tulifanya nini? Tulitaka kuwa kama hao wengine. Sasa tunaona ya kwamba neema ndicho kitu pekee kinachotufanikisha, kamwe si torati.

81 Yoshua hapa ni mfano wa huduma ya siku za mwisho. Mnaona? Sasa kumbukeni hizo hatua tatu za safari. Zote zilikoma, kwanza ilibidi torati na kila kitu kukoma, kusudi Yoshua . . . Nalo *Yoshua* ni neno lile lile kama Yesu, "Yehova-mwokozi," aliyewatoa kutoka nyikani mwao akawaingiza kwenye nchi ya ahadi. Sasa ninajua wengi hushikilia . . .

82 Nami sitaki kupingana na wasomi, bali wengi wanashikilia ya kwamba nchi ya ahadi inawakilisha Mbinguni. Isingeweza kuwakilisha Mbinguni. Isingeweza, kwa kuwa walikuwa na vita,

na matatizo, na vurugu, na kila kitu, kwenye nchi ya ahadi. Haiwakilishi Nchi ya ahadi.

83 Lakini mnaona, kabla tu hawajaingia kwenye nchi ya ahadi, to—tofauti zote ambazo—ambazo zilikuwa zimeibuka miongoni mwao. Walininii . . . Moja ya mambo makuu lilikuwa ni Kora. Hakutaka uongozi huu wa mtu mmoja. Dathani, na jinsi walivyojitokeza mbele ya Musa na kujaribu kumwambia ya kwamba "ilibidi u—ujumbe umaanishe *hili*," na kuweka tafsiri tofauti kwake, mawazo yao wenyewe ya kile lilichokuwa. Basi kila mmoja wao akaangamia! Kila mmoja!

Yesu alisema, "Wote waliangamia."

84 Wakasema, "Baba zetu walikula mana nyikani, kwa muda wa miaka arobaini," Yohana Mtakatifu 6.

Yesu akasema, "Na kila mmoja wao amekufa."

85 *Kufa* linamaanisha "Kutenganishwa Milele." Wote wamekufa, hata hivyo walifurahia kuusikia ujumbe, hata hivyo walifurahia mana iliyoshuka. Sio mana nyingine; mana halisi!

86 Lakini ilipofikia wakati ambapo Balaamu alijitokeza na fundisho lake la uongo, na kusema, "Sisi sote ni mmoja. Kwa nini tusiende tu pamoja na kuacha watoto wetu waoane? Sisi ni taifa kuu. Tutawafanya wakuu pamoja na sisi." Sasa mtu yeyote mwenye ufahamu wa kawaida wa kiroho anaweza kuona jambo lile lile hata leo, kuwaunganisha wote pamoja. Nayo ilikuwa ni dhambi isiyosameheka. Haikusamehewa Israeli kamwe.

Lakini basi Yoshua akainuka kwa ajili ya kutoka.

87 Sasa tunafundishwa, katika Ufunuo mlango wa 6, ninaamini, naam, mlango wa 6, wa ile Mihuri Saba. Hiyo inapaswa . . . Kitabu hicho kufungwa kwa siri saba, ama Mihuri Saba, Ufunuo 6. Na katika siku ya mwisho, Ufunuo 10, katika Ufunuo 10, tunaona ya kwamba Laodikia, mjumbe wa mwisho wa wakati wa mwisho, na kwenye wakati wa unabii wake, ya kwamba Mihuri Saba ingefunguliwa, zile siri saba, siri zenye sehemu saba zilizokuwa zimeachwa.

88 Katika kila wakati kulikuwako na sehemu Yake iliyoachwa. Mtengenezaji hakuwa na wakati wa kuishughulikia. Katika siku za Luther, yeye alihubiri tu kuhesabiwa haki kwa imani. Akaondoka, wakaunda kanisa. Kisha akaja Wesley, akahubiri utakaso. Huo hapo. Ndipo wakaja Wapentekoste.

89 Lakini tumeahidiwa, kulingana na Ufunuo 10, na kulingana na Malaki 4, na Luka Mtakatifu 22:17, na kadhalika, ya kwamba hapana budi Wa—Waefeso ije kwenye huu. Hiyo hapo imeahidiwa, enyi marafiki. Hapana budi Waefeso ije, na hizi siri zenye sehemu saba za Neno la Mungu hazina budi kufunuliwa. Na haya yanatukia katika wakati wa Laodikia. Ninaamini ya kwamba tuko—tuko hapo.

90 Ninaamini tuko hasa kwenye vivuli vya Kuja kwa Mwana wa Mungu. Na kama vile Yoshua, kabla tu Waefeso kutokea, vivyo hivyo Yohana Mbatizaji alitokea kabla tu ya Waefeso nyingine. Nasi tumeahidiwa nyingine, Waefeso nyingine. Imebashiriwa hapa katika Maandiko, kwa hiyo nawaza ya kwamba tunaishi katika Waefeso tena. Kurudi tena kwenye . . . Tumeahidiwa hayo yaliyoachiliwa kwenye nyakati hizo saba.

91 Sasa huwezi kuongeza chochote kwenye Kitabu hicho, wala kuondoa chochote kutoka Kwake. Ufunuo 22:18 yasema hivyo, "Atakayethubutu, atakayeongeza neno moja, au kuondoa Neno moja, ataondolewa sehemu yake katika Kitabu cha Uzima." Sasa hatuwezi kuongeza wala kuondoa.

92 Kwa hiyo basi tunajua ya kwamba Luther asingeweza kulifikia; Wesley, na kadhalika, wale watengenezaji, Knox, Finney, Calvin, na kuendelea, na kadhalika, hawakulipata lote, bali waliyokuwa nayo ilikuwa ni Kweli ya Injili.

93 Lakini sasa katika siku za mwisho, tumefahamishwa, na Neno, ya kwamba tutalifahamu, kwa kuwa utakuja wakati wa Waefeso kwake. Nasi tumewasili! Sasa, kitendawili! Nitaachilia hilo lining'inie, kwa kuwa nina yapata tu dakika kumi zaidi kisha tutafanya mstari wa maombi. Kitendawili!

94 Kuna baadhi ya watu, wa siku hizi, wasioamini miujiza. Wanasema kamwe "hawawezi kuamini ya kwamba kuna kitu kama miujiza katika wakati huu wa kisasa." Vema, sikusudii kusema chochote kibaya kuhusu mtu huyo, bali hao wamekufa ganzi kiroho. Hao, hao, hao ni—hao ni vipofu kiroho. Hawana macho ya kiroho wala hisi za kiroho, hata kidogo. Maana, hakuna mtu anayeweza kuketi kwenye umati wa watu, ambamo Roho Mtakatifu anashuka, haidhuru mwanamume huyo ni mwenye dhambi kabisa, ama mwanamke huyo, pasipo kulazimika kuuhisi Uwepo wa Mungu, mnapoliona Neno aliloahidi likitimizwa. Basi itabidi uwe umekufa ganzi; na unapoyaona kwa macho yako mwenyewe, yakitukia, basi itakubidi kuwa kipofu, kiroho, sineni kimwili. Lakini hakika unaweza ukawa kipofu kiroho, na kuwa na ishirini kwa ishirini, macho ya kimwili.

95 Mnamkumbuka Eliya kule chini Do—Dothani, wakati alipotoka na kulipofusha jeshi zima? Biblia ilisema alifanya hivyo. Ndipo akawaongoza moja kwa moja kwenye uvizio, ambapo hawakujua kwamba yeye alikuwa ni nani. Na hata hivyo sura yake ilikuwa tu jinsi inavyopaswa kuwa, na kadhalika, naye akaenda moja kwa moja kwao. Bali walikuwa ni vipofu.

96 Nawe unaweza kusimama katika Uwepo wa Mungu aliye hai, unaweza kusimama chini ya upako wa Roho na kumwona akitenda kazi, na hata hivyo Huyo hatakugusa. Unaweza kuona yale Mungu aliyosema, yakihubiriwa kwako kikamilifu na kudhihirishwa, na hata hivyo hutaingia, "siliamini," basi,

hapo, huwezi kufikika. Umekufa tayari, umekufa ganzi, umepofushwa, umekwisha. Walikuwa hivyo kabisa.

97 Ulimwengu. Nashangaa, kama mtu yuyo huyo asiyeamini katika mwujiza, sijui na kama yawezekana kwamba vitu pekee vinavyoweza, vilivyo halisi, ni vile vinavyoweza kuthibitishwa kisayansi? Sijui kama ungeweza kuwa na mwanasayansi yeyote, ama mtu yeyote asiyeamini katika mwujiza, kunielezea jinsi ulimwengu huu unavyosimama katika mzingo wake. Unadumishaje wakati wake mkamilifu, kuizunguka ikweta na vile unavyoenda, na ni mkamilifu kabisa? Hatuna mtambo, saa, au aina yoyote, inayoweza kudumisha wakati jinsi hiyo; itaachana kwa dakika chache kila mwezi. Lakini lile jua halichelewi kamwe. Maelfu ya miaka yanapita, halisogei; hakika, kikamilifu.

98 Jinsi ambavyo mwezi, mabilioni ya maili kutoka ardhini, ungali unaweza kudhibiti kupwa na kujaa kwa maji. Niambieni ambavyo katika kundi hili la nyota tunamoishi, mwezi ungewezaje kuathiri maji duniani? Kisayansi, niambieni jinsi hilo linavyotukia. Isingewezekana, kwa maana hakuna njia yoyote ya kisayansi ya kulielezea. Bali Mungu aliuweka mwezi upate kuilinda bahari. Basi mwezi unapoanza kugeuka, dunia inapoondoka, hapa kwaja kupwa na kujaa. Lakini inapoamka, kesho yake asubuhi, ikiangalia *huku* nyuma, maji yanarudi mahali pake tena. Ni mlinzi.

"Loo," unasema, "hiyo ni kwenye ufuko tu wa bahari." La.

99 Hiyo ni papa hapa Arizona, moja kwa moja huko kwenye mkoa wa Kentucky, popote unapochimba shimo ardhini chini vya kutosha kupata maji ya chumvi. Utaona, maji yanapokupwa, hayo maji ya chumvi yanashuka kwenye bomba. Ndipo maji yakijaa, hayo pia yanapanda, mamia ya maili kutoka ufukoni mwa bahari.

100 Tungeweza kuhubiri somo juu ya hilo. Jinsi ambavyo Mungu, haidhuru, Yeye yuko Utukufuni bali maagizo Yake kule yana matokeo yale yale ulimwenguni mwote na mtu yeyote anayeichukua ahadi hiyo. Agizo Lake linatolewa. Yeye ana kanuni za maumbile, na—nazo—nazo zitajiendeleza kikamilifu, kutoka kwenye Pentekoste ama wakati mwingine wowote. Wakati wowote ambapo Mungu alitoa ahadi, Yeye angali atadumu na ahadi hiyo haidhuru watu wako mahali gani, wako umbali wa elfu ngapi za miaka. Kanuni Zake zinabaki zile zile.

101 Jinsi ambavyo mbegu huanguka ardhini, ikaoza, na kutoa uhai tena. Inaonekana kama, endapo italeta uhai kamwe, ingekuwa ni wakati ikiwa katika umbo lake kamili. Kama uhai ulipata kuwa ndani yake, basi kwa nini usichipuke tu? Iingize ardhini, uhai unachipuka. Ni kwa nini yote yanayouzunguka uhai huo, yote yaliyo karibu na chembe hai hiyo ambayo hamna mwanadamu anayeweza kuipata, ni kwa nini kila

kitu kinachoshikika karibu na chembe hiyo hai hakina budi kufa? Ipate kuchipuka katika maisha mapya. Lakini kila kitu kinachoizunguka hakina budi kufa pia na kuoza, kabla haijachipusha uhai.

102 Ndivyo ilivyo kwa mtu binafsi. Mradi tu kuna nyongeza za mwanadamu, mawazo ya mwanadamu, basi chembe ya uhai wa Mungu, Roho Mtakatifu, haiwezi kutenda kazi. Huwezi kuponywa mradi kuna se—sehemu ndogo tu mahali fulani, ambayo bado haijaoza; ina elementi zote za binadamu, mawazo yote ya kisayansi, yote kuhusu "siku za miujiza zimepita," wanavyosema. Yote hayo hayana budi, yote, sio tu kufa, bali kuoza, kisha kutoka hapo hiyo chembe ya Uzima inakua ikawa ni maisha mapya. Hivyo tu ndivyo inavyoweza kukua.

103 Hiyo ndiyo sababu hatupati tunachoomba. Tunajaribu kujitwika, kwa nafsi zetu, mengi sana ya mawazo yetu wenyewe.

104 Hiyo ndiyo sababu kanisa la Kilutheri lisingeweza kwenda mbele zaidi ya lilivyofanya, Wapentekoste na hayo mengine; maana wanaingiza, kwa kundi la wanathiolojia, "*Hili* halipaswi kuwa namna hii. *Hili* ni kwa ajili ya wakati mwingine. Na *Hili* lilikuwa ni kwa ajili ya lile." Linabaki hapo. Haliwezi kukua kuifikia ile sura halisi ya Kristo mpaka kila Neno limepokewa ndani yenu, ndipo mnakuwa hilo Neno. Ni kama mbegu iliyoingia ardhini.

105 Ningewataka waelezee Waebrania 11:3. Mwanasayansi mashuhuri kuliko wote tuliopata kuwa nao, nijuavyo mimi, alikuwa ni Einstein. Wakati ambapo alikuwa hapa si muda mrefu uliopita, katika New York, nilikuwa nikisikiliza kile alichokuwa amesema. Naye alikuwa akizungumza juu ya kundi la nyota, na jinsi zilivyokuwa mbali, naye akathibitisha kwamba kulikuwako na Umilele. Jinsi ambavyo mtu, akienda maili milioni nyingi sana kwa saa, ingemchukua nyingi sana, ama maili milioni moja ya mbio za miaka ya nuru kwa saa, ingemchukua miaka mingi sana kufika kule, laki moja, laki tatu ama kitu kama hicho, na kisha laki tatu kurudi. Kisha akathibitisha kwa njia hiyo, kwa namna fulani, ya kwamba mtu huyo alikuwa tu ameondoka duniani kwa muda wa miaka hamsini! Umilele!

106 Na hilo ni kundi dogo tu la nyota, ambako Mungu alizipulizia kutoka mkononi Mwake! Biblia ilisema! Naye Einstein hatimaye akamalizia na huu, "Kuna njia moja tu ambayo mtu yeyote anaweza kuelezea asili ya ulimwengu huu, hiyo inapatikana katika Waebrania 11:3. 'Tunafahamu ya kwamba ulimwengu uliumbwa pamoja kwa Neno la Mungu.'" Hiyo ni kweli kabisa. Sayansi haiwezi hata kuligusa. Halafu mnasema hamwamini katika muujiza? Ungefanyaje jambo hilo?

107 Mwanasayansi yeyote angaliwezaje kuielezea mvua ya Nuhu, wakati kamwe hakukuanguka tone la mvua juu ya nchi

mpaka kwenye siku hiyo? Bali Nuhu alisema kungekuwako na mvua! Ndipo mvua ya Nuhu ilipokuja, kinyume na sayansi yote; hakukuwako na mawingu yoyote huko juu, hakukuwahi kuwako kamwe na mvua yoyote huko juu. Wangeweza kuthibitisha ya kwamba hakukuwako na mvua yoyote kule juu. Ndipo wakati Mungu alipozifungua mbingu na kuimwaga gha—gharika iliyoifagilia mbali dunia, hicho kilikuwa ni kitendawili; jinsi ambavyo hakika halieleweki, halielezeki. Bali tunajua ya kwamba Mungu alifanya hivyo, kwa maana Biblia ilisema hivyo. Nasi tuna ushahidi duniani, leo hii, ya kwamba ndivyo ilivyokuwa. Mungu alifanya hivyo. Hicho kilikuwa ni kitendawili.

108 Wakati Mungu alipomchukua mzee, jina lake Ibrahimu, kwenye umri wa miaka sabini na mitano; na mkewe, sitini na mitano, miaka mingi kupita wakati wa maisha, kukoma hedhi. Basi wakati alipomchukua mtu huyo na kumpa ahadi, kwenye umri wa miaka sabini na mitano; kwa mwanamke huyu aliyekuwa amemwoa, dada ya—yake wa kambo. Naye alikuwa ameishi naye tangu alipokuwa msichana; walifunga ndoa wakati labda alipokuwa msichana ti—tineja, na hapa alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano. Ndipo akasema, "Utampata mtoto kwa mwanamke huyu."

109 Na vipi kama Ibrahimu angalisema, "Si—si—siamini katika vitendawili. Kamwe si—siwezi kukubali hayo"? Kamwe lisingalitukia.

110 Lakini, unaona, unaposema unaamini chochote, basi inakubidi kuliweka katika matendo. Basi Ibrahimu aliamriwa kujitenga na kutokuamini kwote, na kutembea pamoja na Mungu peke yake. Na badala ya kuwa mnyonge, alitiwa nguvu. Na wakati alipokuwa na umri wa miaka mia moja, naye Sara tisini, mtoto huyo akaja.

111 Ibrahimu angewezaje kumchukua mtoto wake, huko nyuma kwenye safari ya siku tatu, labda maili tisini kutoka kwenye ustaarabu wowote, juu ya mlima ambao Mungu alimwonyesha, aende akamtoe mwanawe mwenyewe, Isaka? Isaka huku akipanda amebeba kuni, tujuavyo sisi, ambaye ni mfano wa Kristo. Na juu ya mlima huu alikuwa amtoe Isaka kama dhabihu, na hapo alipotimiza kila kitu ambacho Mungu alimwambia ila kuchoma kisu mwanawe hata kufa, kupitia kwenye koo lake, hapo alipokichomoa kisu kutoka kwenye ala yake na kuinua mkono wake apate kumtii Mungu, kwa neno! Kwa maana Biblia ilisema, kwamba, "Yeye alijua Mungu asingeweza kufanya ahadi pasipo kuitimiza. Naye alimpokea kama mtu aliyetoka katika wafu, kwamba aliweza kumfufua katika wafu na kumkabidhi huyo tena."

112 Ndipo alipokuwa tayari kumtii Mungu, kwa utimilifu wake, aliushika mkono wake na kusema, "Ondoa mkono wako,

Ibrahimu." Naye huyu hapa kondoo dume aliyeshikwa nyikani, kwenye matawi, kwa pembe zake, juu ya mlima huo, ambako kuna simba, mbwa mwitu, fisi, mbweha, na wanyama wakali wakubwa mno wanaowala kondoo. Halafu alikuwa huko juu kabisa mlimani ambako hamna maji. Kondoo huyo dume alipandaje kule? Ibrahimu alikuwa ameokota mawe kila mahali, kujenga ma—madhabahu. Lakini huyo hapo kondoo-dume, hata hivyo. Hicho kilikuwa ni kitendawili.

113 Na mtu yeyote anayemwamini Mungu na kuliamini Neno Lake, haidhuru hali ya mambo ikoje, Mungu atafanya kitendawili kingine, apate kulitimiza Neno Lake. Kwa kuwa, Ibrahimu alipaita mahali hapo *Yehova-yire*, "Bwana amejitolea Mwenyewe dhabihu." Angali anaweza kusababisha kitendawili kutukia. Anaweza kufanya hivyo alasiri ya leo, kama utaliamini tu Neno Lake.

114 Danieli, kutoka kwenye tundu—tundu lililojaa simba wenye njaa, ingewezekanaje kwamba mtu huyo. . .Ingewezekanaje kwamba mtu huyo, kwenye kundi la simba wenye njaa, alikaa kwenye pango hilo pamoja nao, usiku kucha, pasipo madhara yoyote? Malaika wa Bwana, asiyeonekana na mtu mwingine yeyote, alikuwa amesimama pale. Ilikuwa ni kitendawili. Ilibidi kitu fulani kumzuia simba huyo asimfikie.

115 Wakati wale wana wa kiebrania walipoingizwa kwenye tanuru iliyowaka moto, hilo ni kinyume na ufahamu wote wa kisayansi, kwenye wakati huo mkuu. Ilikuwa ni jambo lisilo la kisayansi kwa mtu kutupwa katika tanuru, iliyokuwa, ambamo wale watu waliokuwa wakiwatupa humo waliangamia, nao wakaingia kwenye hiyo tanuru na kuishi kwenye tanuru hiyo kitambo kidogo, na jambo pekee ilichofanya lilikuwa ni kuwafungua minyororo yao. Hicho ni kitendawili. Lilikuwa halielezeki, lisilo la busara, bali hata hivyo ni kweli.

116 Huyu hapa Yoshua, ambaye tunanena habari zake. Jinsi ambavyo mtu huyo, mtu wa kawaida tu ambaye ndiyo kwanza apitie kwenye lu—lu—lundo la kanuni za imani ambazo watu hao walikuwa wametunga, na torati na sherehe, pasipo na kitu ndani yazo kinachosema kuhusu kumpa mtu nguvu kulisimamisha hilo jua. Lakini hapa, akiwa na agizo kutoka kwa Mungu, "Nitakupa kila kipande cha ardhi ambacho nyayo za miguu yako zitakanyaga. Nitakuwako." Naye adui akaangamizwa.

117 Jua lilikuwa likitua. Kama hao wafalme wangalipata wakati wa kujikusanya pamoja tena kesho yake, hakika angaliwapoteza watu. Lakini Yoshua alijua alihitaji mwangaza wa jua. Basi akaliangalia jua, na kusema, "Simama kimya juu ya Gibioni. Na, wewe mwezi, tulia hapo juu ya Aiyaloni." Na kwa muda wa siku nzima, hiyo ilikuwa ni usiku kucha, jua likasimama kimya na mwezi ukasimama pale. Hicho ni kitendawili. Mtu anayetembea katika mapenzi ya Mungu angeweza kufanya jambo kama hilo,

kwa kuwa alikuwa katika ninii...alikuwa tena katika Wa—Waefeso, katika Wa—Waefeso pamoja na—na Injili. Hakika, ilikuwa ni kitendawili.

118 Musa akiwa na kijiti mkononi mwake, kushuka kwenda kuwakomboa wana wa Israeli, ilikuwa ni kitendawili, huku Misri ikiwa na majeshi yote na watu wake waliofunzwa vizuri. Ilikuwa ni kitendawili.

119 Kuzaliwa na bikira kulikuwa ni kitendawili. Bikira angewezaje, kinyume na maarifa yote ya kisayansi, mwanamke asiyemjua mwanamume, angeweza kuzaa mtoto; wala si mtoto tu, bali Imanueli, ambaye alithibitisha kuwa kile hasa lilisema angekuwa. Hiyo ingewezaje kutendeka? Ilikuwa ni kitendawili. Kwa sababu, Mungu alinena na nabii Wake, mamia ya miaka hapo kabla, naye nabii akalitii Neno la Mungu, ndipo Neno likanenwa. "Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu." Nasi tunaamini hilo. Hakika, ilikuwa ni kitendawili.

120 Jinsi ambavyo angeweza kutembea juu ya maji, hicho kilikuwa ni kitendawili. Mwanadamu, kulingana na ukubwa wa miguu yako, asingeweza kufanya hivyo. Lakini alifanya. Ilikuwa ni kitu gani? Halielezeki, bali hata hivyo ilikuwa ni kitendawili. Mungu alifanya jambo hilo. Tunaliamini.

121 Ati kuwalisha watu elfu tano, kwa samaki wawili na biskuti tano? Lakini alifanya hivyo. Akazidisha si samaki tu, bali samaki waliopikwa; sio mkate tu, bali mkate uliookwa. Angewezaje kuyageuza maji yakawa divai? Yote kitendawili!

122 Aliwaponya wagonjwa, ambao, wenye ukoma. Ambao, hawana chochote, hata wa leo, sayansi haina, cha kuuponya ukoma, lakini Yesu aliuponya kwa Neno Lake. Ilikuwa ni kitendawili.

123 Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Neno Lake lingali linawaponya wagonjwa. Ni kitendawili, hakika.

124 Aliwafufua wafu, baada ya uhai wa kibinadamu kuwatoka; Lazaro, yule mwana wa yule mwanamke wa Naini, na binti ya Yairo. Aliwafufua wafu, kwa Neno Lake, kwa maana Yeye ni Neno.

125 Halafu jambo lingine kuu, katika kufunga, kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Kuthibitisha kile alichokuwa, ilibidi aje katika utaratibu, na kutoa jibu, kwa Neno. Nalo Neno lilisema, wakati aliposema na nabii, "Bwana Mungu wako atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi."

126 Kulikuwako na watu wengi walioinuka. Na kulikuwako, kwa mamia na mamia ya miaka, hawakuwa na nabii. Loo, walikuwa na makuhani na watu mashuhuri, na tunaposoma historia katikati ya wakati wa Malaki na Mathayo, miaka mia nne, kulikuwako na watu mashuhuri. Ila hakukuwako na nabii.

127 Ndipo wakati alipojitokeza, kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Waefeso iliyodhihirishwa, Yohana alilitangaza. Bali Yesu alikuwa Ndiye, alikuwa Neno lililodhihirishwa, Yeye Mwenyewe.

128 Wakati Petro alipomjia siku moja, pamoja na Andrea, jina lake lilikuwa ni Simoni. Na wakati Yesu akisimama pale, kamwe hajapata kumwona mtu huyo maishani Mwake, (sikilizeni kwa makini) wakati aliposimama pale na kumwangalia mtu huyo, na kusema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona." Hicho ni kitendawili. Hakika kilikuwa. Hakika kilikuwa ni kitendawili.

129 Na wakati Filipo, akisimama pale, aliposikia hili na kujua kwa utambulisho wote kwamba huyu alikuwa Ndiye Masihi, hakika alikuwa. Aliliamini. Hakuwa amekufa ganzi, wala hakuwa kipofu. Alikimbia ufukoni, kwa maili chache, akampata rafiki yake, jina lake Nathanaeli. Basi wakati alipokaribia akitembea. . .Imani ya mtu huyo, ambaye angeweza kumleta mwingine kwenye mkutano, kuona!

130 Wakati alipoenda mbele za Yesu, Yesu alisema, "Tazama, yule pale Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake."

131 Lilimshtusha mtu huyo. Akasema, "Ulipata kunifahamu lini?" Sasa angalieni, hili si la busara. Hali—halielezeki. Yeye alisema, "Ulinifahamu vipi?"

132 Kasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona." Kitendawili!

133 Alikuwa na haja, kupitia Samaria. Ndipo alipopita Samaria, mji wa Sikari, alikuwa ameketi huko akiwangojea wanafunzi Wake waende wakanunue chakula. Ndipo, angalieni, mwanamke akaja hapo kisimani, mwenye sifa mbaya. Naye akamwambia, "Mwanamke, nichotee maji ninywe, ama nipe maji ninywe."

134 Naye akasema, "Si kawaida Kwako kuomba hayo. Sisi ni, mimi ni Myahudi. . .ama Msamaria, na Wewe ni Myahudi. Hatuna u—uhusiano Nanyi."

135 Akasema, "Laiti ungalijua ni Nani unayesema Naye!" Angalieni kitendawili hiki kikikaribia kutendeka. Msikikose. Kasema, "Wa—wawezaje kufanya, kusema hivi? Mimi, mimi ni mwanamke Msamaria, na Wewe ni Myahudi. Hatuna uhusiano."

136 Akasema, "Lakini kama ungalijua ni Nani unayesema Naye, ama ni Nani anayesema nawe, u—ungeniomba maji unywe." Ndipo akaendelea mpaka akapata shida yake ilikuwa ni ipi. Ndipo akasema, "Nenda kamwite mumeo mje naye hapa."

Naye akasema, "Sina mume yeyote."

137 Akasema, "Hiyo ni kweli. Huna mume, kwa maana umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako. Kwa hiyo, umesema kweli."

138 Akasema, "Bwana, naona ya kuwa U nabii." Hawakuwa wamemwona mmoja kwa mamia ya miaka. Kasema, "Tunajua yuaja Ma—Masihi, na, atakapokuja, Yeye atatwambia mambo haya."

Akasema, "Mimi Ndiye."

139 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Ilikuwa ni kitendawili kilichothibitishwa, na kinathibitika kwamba ni Kweli ya Injili; Injili iliyokuwa imeahidi jambo hili, nalo hili hapa likatukia na kuthibitisha ilichokuwa.

140 Sasa hebu niwape kitendawili kingine kikubwa cha kupendeza hapa, dakika moja tu. Katika Yohana 14:12, Yesu alisema, aliahidi ya kwamba, "Mwaminio aliyemwamini Yeye, angefanya kazi zile zile." Hiyo ni kweli? Mungu, ambaye hufanya torati ama ahadi, hana budi kutimiza ahadi hiyo, apate kuwa Mungu. Yeye huitimiza. Kuwazia, yule Mungu. . . Mbona, Chenyewe, ni kitendawili; kwa Mungu, ambaye hutoa ahadi wala hawezi kuivunja ahadi hiyo, kutoa ahadi hiyo ya mambo aliyofanya, kwa watu Wake, kuyafuata kote katika nyakati mpaka atakaporudi tena. "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe; kila kiumbe, ulimwenguni kote. Aaminiye na kubatizwa ataokoka, na asiyeamini atahukumiwa; na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hana budi kulitimiza hilo Neno. Na kwa kuwa Yeye alilisema, likatoka katika kinywa Chake, halina budi kutimizwa.

141 Maandiko yote hayana budi kutimizwa. Kwa hiyo ni kitendawili, pekee, kumsikia Yesu, Mwana wa Mungu, akitoa tamshi kama hilo, "Mambo niyafanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya." Sasa Biblia ilisema, katika Waebrania 13:8, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Hicho ni kitendawili, maana hayana budi kutimizwa. "Mbingu na nchi zitapita, bali hata Neno moja nililopata kusema halitashindwa," Yeye alisema. Halina budi kutukia.

142 Sasa, enyi marafiki, ninaamini kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ninaamini Yeye anaweza tu alasiri ya leo kusababisha, katika jengo hili, kitendawili, kwa maana aliahidi ingetendeka.

143 Basi ni mengine mengi zaidi jinsi gani Yeye ameahidi, ni zaidi kiasi gani yanayoelekeza katika Biblia, kwenye wakati huu tunaoishi, Waefeso tena, ya nyakati za kanisa. Tuna nyakati saba za kanisa, nasi tumeahidiwa ya kwamba kwenye Wakati wa Kanisa la Laodikia kungekuwako na Waefeso nyingine. Hiyo ni kweli. Nasi tumewasili. Ninaamini, kwa moyo wangu wote, ya kwamba Yesu Kristo aliyefanya ahadi hiyo. . .

144 Kama nilivyosema katika ujumbe wangu wa mwisho, nikisimama pale kuegemea ukuta ule, nilipokuwa hapa majuma machache yaliyopita. Kila unapokisogeza kidole chako, hilo linaizunguka dunia tena na tena, halitakoma kamwe. Kila

hatua unayochukua, utaiona kwenye Hukumu. Televisheni inathibitisha kwamba kiko hapa, kile kiwango cha nne. Hakika, televisheni haiitengenezi picha hiyo, inalielekeza tu hilo wimbi kwenye tyubu, nawe unaona picha. Rangi, kila kitu, kila kitu kinachosogea ambacho kinatukia ulimwenguni, kinazunguka-zunguka papa hapa sasa, kikiandika kumbukumbu. Siku moja, kumbukumbu yako itafungwa, nawe utawajibika kwa kumbukumbu hiyo. Hiyo ni kweli.

145 Mungu, jalia niunganishwe kabisa, jalia nife kabisa kwa nafsi yangu na chochote kinachonizunguka, bali nilitambue Neno la Mungu linaloishi miongoni mwetu leo hii!

Na tuombe.

146 Bwana Yesu, Wewe ni kitendawili, wakati Mungu alipofanyika mwili. Ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utajidhihirisha Mwenyewe alasiri ya leo, ukituthibitishia hapa leo hii. Sio tu kututhibitishia...Kunao, nadhani, asilimia tisini, ama zaidi, ya watu wanaoketi hapa, wanaamini hilo, kila Neno. Bali ili tukuone tena, na utujalie kujua ya kwamba Neno hili ulilonena, ambalo lingali linasafiri kuzunguka na kuzunguka ulimwenguni, kama tu kumbukumbu, jalia tuingie kwenye kumbukumbu hiyo, leo hii, Bwana. Jalia tuingie ndani wala tusilisikie kana kwamba tu lilikuwa likija kupitia kwa mwingine, kutoka kwenye kinywa cha mwanadamu; bali jalia kinywa hicho, na mtu na watu, wote wanaoketi hapa, wafanyike Neno Lako. Tuko tayari kufa, Bwana, kwa mawazo yetu wenyewe, kukuona tu ukiitimiza ahadi Yako, "Mambo nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya pia." Ninaomba ya kwamba utalijalia hili katika Jina la Yesu. Amina.

147 Kabla tu hatujaufanyiza mstari wa maombi. Nilikuwa nikimenya kipande kidogo cha aiskirimu siku moja, pamoja na maskini daktari rafiki yangu. Akasema, "Nataka kukuuliza jambo fulani, Billy."

Nikasema, "Vema."

148 Kasema, "Je! unaamini katika..." Hapo ndipo nilipopata wazo hili, *kitendawili*. Kasema, "Je! unaamini katika kitendawili?"

Nikasema, "Hakika."

149 Akasema, "Na—najua unaamini." Akasema, akaniambia kuhusu mtu fulani aliyekuwa ameponywa, alikuwa ameombewa; ambaye alikuwa amemwuzia dawa za kifafa, kwa miaka kadha, wakati mwingine wangeshikwa na kifafa mara saba ama mara nane kwa siku; dawa kali. Naye akasema, "Kamwe hawakurudi kununua zingine. Nami huwaona wakati wote; kamwe hawakushikwa nacho tena." Kasema, "Nataka kukwambia jambo fulani, kukufanya tu ujue ni—ninaamini kile unachozungumzia."

150 Akasema, “Katika wakati wa kuzorota kwa uchumi, mwanangu hapa sasa alikuwa huko dukani.” Kasema, “Kwa namna fulani a—alikuwa akimngojea kijana fulani, alisema tu yeye. . . Walikuwa wamesimama chini mstarini, wapate dawa.” Kisha kasema, “Mtu mmoja alisogea hapa mbele, naye alikuwa na mke wake,” kasema, “maskini mwanamke mdogo, alikuwa. . . Ungeweza kumwangalia na kuona alikuwa karibu tu na kujifungua wakati wowote, mtoto.” Naye akasema, “Asingeweza kusimama kwenye mstari huo tena, kwa hiyo a—akamleta mkewe mlangoni, naye anaegemea tu begani mwake.”

151 Ndipo kasema, “Mvulana wangu akaenda pale, kasema, ‘Naweza kukusaidia?’ Kasema, ‘Naam,’ kasema, ‘haya hapa maagizo kutoka kwa daktari. Lakini,’ kasema, ‘nataka kukwambia waziwazi.’ Kasema, ‘Mimi. . . hatujapata pesa bado.’ Kasema, ‘Tutazipata kutoka wilayani, bali mke wangu kamwe hawezi kuvumilia zaidi. Daktari alisema atapata dawa mara moja.’ Kisha kasema, ‘Kama tu ukimpa dawa, nitaenda moja kwa moja pale na kusimama mstarini mpaka ni—nipate pesa kutoka wilayani.’

152 “Ndipo mvulana huyo akasema, ‘Bwana, samahani.’ Kasema, ‘Ni kinyume na amri ze—zetu hapa, kutoa dawa bila pesa.’ Mnajua jinsi hali ilivyokuwa katika siku hizo. Basi kasema, ‘Na—namwonea huruma, bali siwezi kufanya hivyo.’ ”

153 Kasema, “Nilikuwa nimeketi nyuma hapa nikisoma gazeti. Ndipo nikaangalia juu, na,” kasema, “kitu fulani kikauchochea moto moyo wangu kiajabu.” Kasema, “Nikaenda pale, nikasema, ‘Hebu kidogo, mwanangu, ngoja kidogo.’ Mtu huyo akaanza kutoka mlangoni, akasema, ‘Vema, sawa, mwanangu,’ akaanza kutoka mlangoni.” Naye akasema, “Nikasema, ‘Hebu kidogo,’ kasema, ‘kuna nini?’ Akasema, ‘Vema, mtu huyu. . .’ Akamwelezea.”

154 Akasema, “ ‘Hebu nione maagizo hayo.’ Kasema, ‘Hebu kidogo, mwanangu, nitakupa hizo dawa.’ ”

155 Kasema, “Nikarudi na kuchanganya maagizo hayo daktari alikuwa ameagiza kwenye karatasi yake.” Kisha kasema, “Nikaenda pale, na kuchukua fedha hizo.” Kasema, “Nikamkabidhi, pasipo kujua kama nitazipata ama la, bali niliwazia tu nitazipata.” Kasema, “Nilijisikia tu kwamba inanipasa kufanya hivyo.” Ndipo kasema, “Billy, nilipoziweka hizo—hizo dawa mkononi mwa mwanamke huyo,” kasema, “ilikuwa ni Bwana Yesu.” Kasema, “Nilimwona Mtu amesimama pale.” Naye akasema, “Nilisoma baadaye, ya kwamba Maandiko yalisema, ‘Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hawa, watoto Wangu wadogo, mmenitendea Mimi.’ ” Akasema, “Billy, nini kiliyapata macho yangu? Kweli niliuona?”

156 Nikasema, “Naam, bwana. Ninaamini hilo. Ninaamini kwamba kweli ulitimiza wajibu wako kama mwuza dawa, katika

mahitaji hayo ya dharura. Yesu alisema, 'Uliyowatendea hawa wengine, umenitendea Mimi.' Ninaamini hilo."

157 Nami ninaamini jambo lilo hilo leo, papa hapa akiwepo pamoja na watu hawa, kwamba Yesu Kristo anaweza kujidhihirisha, kujifanya Neno lililofanyika mwili miongoni mwetu alasiri ya leo. Mtaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Bwana awabariki.

158 Sasa tutaziita kadi za maombi, watu wapate kuja. Nasi hatuwezi kuwaleta wengi kupita kiasi, kwa kuwa nawazia sasa, kama ninaangalia saa vizuri, nina dakika ishirini na tano kufikia ambapo itatubidi kufunga kwenye saa kumi kamili, kwenye wakati mzuri, bali tutaendelea. Sasa hebu tuanzie kwenye kadi ya maombi, ninaamini ilikuwa ni A. Sivyo? A, hebu twende kutoka kwenye A, moja.

159 Ni nani aliye na kadi ya maombi A, moja? Tutawaita tu mmoja mmoja, kwa hiyo kama wewe ni mlemavu tunaweza kukubeba. Vema. Kadi ya maombi A, moja. Ni nani aliye nayo, inua mkono wako, mahali fulani humu jengoni? Kadi, huko nyuma kabisa. Naomba uje, mama, ukiweza. Moja, mbili, ni nani aliye na kadi ya maombi mbili? A, mbili, waweza kuinua mkono wako juu kama wewe . . . Je! waweza kutembea? Vema, njoo papa hapa, njoo upande huu. Tatu. Kama utainua mkono wako mara moja, ni—ninaweza kukupata, haitatubidi kungojea muda mrefu sana. Kadi ya maombi namba tatu, naomba uinue mkono wako. Vema, mwanamume fulani huko chini. Vema, njoo huku, bwana.

160 Kadi ya maombi namba nne, naomba uinue mkono wako upesi sasa, upesi tu uwezavyo. Kadi ya maombi namba nne. Vema. Namba tano. Mara tu nikiita, simama, namba tano. Vema. Namba sita, namba saba, namba nane, namba tisa, kumi—kumi. Sasa, moja, mbili, tatu, nne . . . Kumi, vema. Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne. Ulikuwa unakuja, bwana, kumi na nne? Vema. Kumi na nne, kumi na tano. Vema, hao, hao wataninii . . . Hao watatosha sasa hivi, hao watatosha alasiri ya leo, maana hatuna wakati mwingi sana.

161 Sasa angalieni. Ninawatakeni mnipe usikivu wenu wote. Sasa, Yesu alifanya ahadi hii, kwamba, "Kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, ila ninyi mtaniona." Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Ulimwengu," *ulimwengu*, ni "utaratibu wa ulimwengu." Mnaona, ya kwamba, Yeye alijua wangepotea katika mitindo na kadhalika. "Bali hawataniona tena, bali ninyi mtaniona." Kwa kuwa Yeye aliahidi, "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ukamilifu wa dahari." Hiyo ni kweli? ["Amina."] Nayo Biblia ilisema, Waebrania 13:8, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Mnaamini hilo? ["Amina."] Hiyo ni ahadi.

162 Sasa, si lazima uwe hapa juu, upate kuponywa. Jambo pekee linalokupasa kufanya ni kuamini hilo Neno kwamba ni Kweli.

Sasa nitawaombeni, tafadhalini, mwe tu na kicho na kimya kwa dakika chache.

163 Hivi wote waliingia, Billy? Wawili hawako, watatu hawako? Ati nini? [Ndugu mmoja anasema, "Watatu zaidi."—Mh.] Ati watatu zaidi? Namba tatu, kadi ya maombi namba tatu. Inaitwaje, inasemwaje, hiyo inaitwaje kwa Kimeksiko, tatu? Kuna mtu anayeweza kulitamka? [Mtu fulani anasema, "tres."] Vema, hakika walisikia. Ni nani, yule, yeyote aliye na kadi hiyo ya maombi, aingie mstarini, sivyo? Loo, naam. Loo, nafikiri ni mtu fulani aliyekuwa nayo, wala hakujua, nao wakarudi. Vema. Sasa, sasa vipi kuhusu . . .

164 Je! kila mtu sasa anaamini kwa ninii wako wote—kwa moyo wako wote? Vema, na tuombe tena basi.

165 Bwana Yesu, sasa tunatambua ya kwamba tunaweza kusoma Neno, kwa yote tujuayo, kulielezea. Lakini, Bwana, Wewe Ndiye tu unayeweza kulithibitisha. Wewe Ndiwe tu unayeweza kusema ya kwamba ni la kweli ama si kweli. Na, Baba, ninaomba leo ya kwamba utajalia macho ya watu yafunguliwe. Jalia tuone kitendawili alasiri ya leo, ninii tu, Bwana, cha kutosha kuwafanya watu waone kwamba Wewe upo, kwamba wewe hu—hujatoweka, kwamba Neno Lako ni lile lile jana, leo, na hata milele. Kwa kuwa, Wewe Ndiye lile Neno. Kwa ajili ya wagonjwa, Bwana, kwa ajili ya wale wanaoteseka; wengi labda wako hapa kutoka sehemu mbalimbali nchini, sehemu za taifa hili, hawana budi . . . wanateseka sana, wasingeweza kuifurahia mikutano, vinginevyo, kama wasingeponywa. Ninaomba ya kwamba utawaponya. Tujalie, Bwana. Na sasa sisi ni wanadamu tu kimwili, na tunaweza tu kulihubiri Neno na kusema yale uliyosema kwamba ni Kweli, sasa Wewe Ndiye wa kulifanya halisi. Ninaomba ya kwamba utatujalia, katika Jina la Yesu. Amina.

166 Sasa ningetaka mnisikilize kwa makini, kwa dakika moja tu, na kama kila mtu ataketi tu sasa kwa dakika chache. Sasa, nijuavyo mimi, hakika, sijui mtu yeyote ninayeweza kumwona humu je—jengoni, ambaye ningemfahamu huko nje. Sasa, haikubidi kuwa hapa upate kuponywa, mtu yeyote anajua hilo. Mnaona?

167 Kulikuwako na maskini mwanamke mmoja, wakati mmoja, asingeweza kupata kadi ya maombi, tuseme, naye akagusa vazi Lake. Ndipo akageuka akaangalia, na kusema, "Ni nani aliyenigusa?" Nao wote wakakana. Basi akaangalia kote na akamwona maskini mwanamke huyu. Asingeweza kujificha, maana, mnaona, Roho wa Mungu, aliyekuwa ndani Yake, alimwongoza. Yeye alikuwa ni Neno. Nalo likamwongoza mpaka kwake, ndipo akamwambia shida yake ilikuwa nini. Alikuwa akitokwa na damu, naye akaponywa. Akaamini. Ndipo mara, mwilini mwake, akajisikia ya kwamba kutokwa kwake na damu

kulikuwa kumezuiliwa, (hiyo ni kweli?) kulikuwa kumekoma papo hapo.

168 Sasa Yeye ni yeye yule tu leo. Si lazima uwe hapa. Sasa, Biblia ilisema ya kwamba katika Agano Jipya sasa, kwamba, "Yesu Kristo Ndiye Kuhani wetu Mkuu." Je! tunaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kuhani Mkuu pekee tuliye Naye, Mpatanishi wa pekee tuliye naye kati ya Mungu na mwanadamu, ni Mwanadamu, Kristo Yesu. Mnaamini hilo? ["Amina."] Nayo Biblia ilisema, "Yeye ni kuhani Mkuu anayeweza kuchukuliana nasi katika udhaifu wetu." Hiyo ni kweli? ["Amina."] Ni wangapi wanaojua hilo ni kweli? Inua mkono wako kusudi waninii . . . Vema. Siko miongoni mwa wageni, kwenye Neno hili.

169 Sasa Yeye angetenda jinsi gani kama ungalimgusa? Angetenda jinsi alivyotenda wakati alipokuwa hapa, kwa kuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

170 Sasa amini tu. Sema tu, "Sasa, Bwana, nimekuwa kwenye mikutano niliyohudhuria, lakini nitaamini tu, leo. Hata si—sitajisumbua. Nitaamini tu kwa moyo wangu wote, ya kwamba Wewe upo hapa. Nami nina haja, Nawe unaninii tu . . . Nisaidie, Bwana." Mnaona? Sasa fanyeni hivyo. Msiwe na wasiwasi; tu—tulieni tu kwa uaminifu.

171 Karama ya imani si kitu unachokichukua na kufanya jambo fulani nacho. Karama ya imani ni wewe kujiondoa tu njiani. Karama ni kujiondoa njiani.

172 Sasa huyu hapa mwanamke amesimama. Mungu Baba anajua, kadiri nilivyowahi kujua, kamwe sijapata kumwona mwanamke huyu maishani mwangu. Yeye ni mgeni kabisa kwangu. Lakini, wala hakuna yapata watu wawili ama watatu ninaoweza kuwaona huko, niwajuao.

173 Nafikiri huyu ni Bibi Vayle anayeketi hapa, mke wa Ndugu Lee. Sina hakika. Halafu ninawajua wavulana hawa watatu ama wanne wanaoketi papa hapa. Nijuavyo mimi, hao tu ndio ninaoweza kuona mkutanoni wakati huu, niwajuao. Ninaamini yule ni Ndugu Anthony Milano anayeketi pale, kutoka New York. Ndugu Pat Tyler kutoka Kentucky. Nje ya hao . . . Ninajua Fred Sothmann yumo mle mahali fulani, nilimsikia akisema "amina" kwa sauti kuu muda mfupi uliopita. Hao, hao ndio pekee, Naye Baba wa Mbinguni anajua hilo.

174 Naye mwanamke huyu anayesimama hapa, wala sijapata kumwona. Sina fununu yupo hapa kwa sababu gani. Yeye ni mwanamke tu aliyepanda hapa jukwaani, kama tu vile ninyi mmeketi hapo.

175 Sasa, kama mwanamke huyu ana haja, vema, basi mimi—mimi, kama ningeweza kumsaidia, hakika ni—ningemsaidia. Lakini sasa mimi—mimi . . . Hiyo inategemea ana haja gani.

Kama ilikuwa ni pesa, huenda ni—nikajitahidi sana kumtafutia dola tano ama kumi. Nje ya hizo, sijui, mnaona, isipokuwa nimpe hundi ya baadaye, mpaka nitakapopata mshahara wangu mwezi ujao. Lakini sasa vipi kama ana shida ya kinyumbani? Basi ningesema, "Nenda kamlete mumeo, tuzungumze pamoja, labda ninaweza kuwasaidia. 'Sina njia ya kufika nyumbani'? Vema, nitamwomba mtu fulani kama watakupeleka, wakupeleke nyumbani, wanaopitia njia yako. Unaishi kwenye mtaa gani hapa chini?" Ama chochote kile, sijui. Lakini kama ni maradhi, basi si—sijui mimi. Mnaona? Bali simjui mwanamke huyu.

176 Bali yupo mtu Fulani hapa, Neno hili, aliyeahidi, "Mambo nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya."

177 Sasa, labda, vipi kama mwanamke huyu ni mgonjwa, labda yuna kansa, labda yuna TB, na, ama kitu ambacho dawa haziwezi kusaidia katika ha—hatua hii? Vema, sasa, nisingeweza, nisingeweza kwa njia yoyote kumponya mwanamke huyu.

178 Lakini sasa kama anaweza kunifunulia yale anayotaka, kama tu alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, ama kama alivyomwambia Nathanaeli, ama—ama alivyomwambia Simoni kwamba jina lake lilikuwa ni nani. Kasema, "Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona. Tangu sasa utaitwa *Petro*, ambalo linamaanisha 'jiwe dogo.'"

179 Vema, sasa, kama angefanya jambo kama hilo hapa mbele zenu ninyi nyote, hiyo inaonyesha ya kwamba Neno hilo ni Kweli. Sasa, ni wangapi watakaoamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yupo mtu yeyote hapa anayemfahamu mwanamke huyu, inua mkono wako, watu wowote humu jengoni? Naam, wengi wenu mnamfahamu. Vema. Naye Baba anajua kwamba simjui. Vema, sasa, hebu tuone tu yale Yeye angesema. Na hilo, je! hilo lingekuwa ni kitendawili? ["Amina."] Sijui ana shida gani. Sijui kilichomleta hapa, wala chochote kumhusu. Lakini Mungu anajua hilo.

180 Nitazungumza na mwanamke huyu. Sasa huyu ndiye mtu wa kwanza nimekuwa naye mbele zangu, kwa yapata miezi mitatu. Sasa ninataka tu kuzungumza na mama huyu, kwa dakika moja tu. Na hiyo ni nini? Kuwasiliana na roho yake. Kama tu vile Yesu alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, kuwasiliana na roho yake.

181 Sasa, kama Bwana Yesu, mama, anaweza kunifunulia shida yako, ama kilichokuleta hapa, ama jambo fulani kukihusu, ambalo unajua ya kwamba sijui lolote kulihusu, ama kitu kama hicho, je! ungeamini ilikuwa ni Yeye? Ingebidi iwe ni Yeye, sivyo? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Ingebidi iwe ni Yeye. Kama atafanya hilo, basi sote tutashukuru kwamba tunajua tunaninii. . .kwamba Neno Lake ni la kweli, basi tunaweza kuweka matumaini yetu kwake.

182 Sasa, kama anaweza kufunua shida yako ni gani, kunifunulia mimi, nami sikujui, nawe unajua hilo; bali sasa kama Yeye anaweza kunifunulia shida yako ni nini, ama jambo fulani kukuhusu wewe, basi hiyo inaonyesha kwamba kuna Roho fulani hapa, mahali fulani, anayekujua, nawe unajua kwamba sikujui. Kwa hiyo haingekuwa ni mtu huyo, ingekuwa ni Roho. Na hayo ndiyo Mungu aliyoahidi kwenye wakati huu wa Waefeso. Unaamini hilo kuwa ni Kweli? [Huyo dada anasema, "Ndiyo, ninaamini."—Mh.] Na alijalie.

183 Ninaona jambo moja, anaugua kitu kama uvimbe *hapa* juu kichwani mwake. Hiyo ni kweli. Sivyo? Inua mkono wako kama ndivyo ilivyo. Lakini uvimbe usingekufanya upige chafya na kuteseka jinsi hiyo, kwa hiyo una homa iletwayo na vumbi, pia. Hiyo ni kweli. Hutoki Phoenix. Umetoka mahali penye—penye vilima vingi, miti. Umetoka Flagstaff. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Wewe ni Bibi Earl. Naam. ["Kweli."] Hiyo ni kweli, sivyo? Sasa nenda, ukiamini, yote yatakwisha.

184 Sasa je! Yeye ni yeye yule jana, leo na hata milele? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa, Baba wa Mbinguni anajua ndio kwanza tu nimwone mwanamke huyo. Angalieni Neno limethibitishwa. Sasa, sio mimi, mimi ni mwanadamu tu. Kama tu maikrofoni hii, ni bubu pasipo mimi kuzungumza kuipitia, ama mtu fulani. Na vivyo hivyo mtu ni bubu tu. Lakini ni Roho, Naye huyo Roho yumo mumo humo miongoni mwenu. Mnaona? Yeye Ndiye Mponyaji, sio mimi.

185 U hali gani, bwana? Mtu mwingine ambaye ni mgeni kwangu. Simjui mtu huyu. Sasa, nijuavyo mimi, sijapata kumwona maishani mwangu.

186 Lakini sasa Roho, Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu na Yesu Kristo ni Roho yeye yule. Aliyepakwa mafuta, Yesu, Mwanadamu, alikuwa ni Mwana wa Mungu, bali Roho Mtakatifu aliyekuwa juu Yake alikuwa ni Mungu. "Baba Yangu anakaa ndani Yangu." Mnaona, ni Roho Mtakatifu, kwa hiyo angali ni Mungu.

187 Sasa kama ningeweza tu kuninii, kama mtu huyo angeweza, kujiondoa njiani, basi sehemu hiyo imekufa, basi acha Roho wa Uzima aanze kutenda kazi. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu mimi hungojea kidogo tu, kuona kile kinachotukia mpaka upako unapoanza.

188 Kama Bwana Mungu, ambaye tuko katika Uwepo Wake, atanifunulia, bwana, shida yako ni nini, ama kitu fulani ambacho umefanya, ama—ama jambo fulani kukuhusu wewe, jambo fulani tu. Hakika, kadiri tungezungumza mengi, ndivyo yangefunuliwa mengi. Lakini, unaona, wapo wengine wanaosimama mstarini. Lakini kama ataniambia tu shida yako ni nini, je! utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake, na kuamini

Yeye yupo? [Ndugu huyo anasema, “Naam.”—Mh.] Henia. Hiyo ni kweli? [“Hakika ni kweli. Naam.”] Kweli.

189 Sasa unasema, “Hilo lilifanyikaje?” Laiti ningalijua. Hakuna mtu anayeweza kulielezea hilo. Hicho ni kitendawili. Mnaona?

190 Hapa, kusudi upate kujua, nimeona kitu kingine, kuchunguzwa; una ugonjwa wa moyo, pia. Inua mkono wako. Bw. Anderson, unaweza kwenda nyumbani sasa, Yesu Kristo atakupa afya. Hiyo ni kweli. Amini tu, kuwa na imani. Usitie shaka.

191 U hali gani, bwana? Hatufahamiani. Sikujui. Nijuavyo mimi, ni mara ya kwanza niliyopata kukuona, kukujua. Hiyo ni kweli. Lakini Yeye anatujua, sote wawili.

192 Sasa mnajua ni kwa nini haya yanatukia? Ni neema Yake inayoliruhusu, ipate kuwafanya watu hawa wamjue Mungu. Sasa, huku sijui lolote kukuhusu, sikujui kabisa, ni mgeni tu ambaye amekuja hapa. Sasa ingekuwa ni kitendawili kabisa kwa jambo fulani kutukia, ku—kujua ulikuwa na shida gani, ama jambo fulani ulilokuwa umefanya, ama jambo fulani usilopaswa kufanya, ama jambo fulani ulilopaswa kufanya, ama wewe u nani ama jambo fulani kukuhusu. Ingebidi iwe ni kitendawili, maana hakuna njia mtu yeyote anaweza kujua hilo, nje ya ufunuo fulani wa yasiyoonekana. Hiyo ni kweli. Sasa kama Yeye atakufanyia hilo, kati yako na mimi, ili kwamba wasikilizaji . . . sio maonyesho, bali kwamba wapate kuona Wa—Waefeso iko hapa, kwamba hiki ndicho kitu kinachounganisha dhehebu na Nchi yenye Utukufu. Yeye aliliahidi, wapate kuhakikishiwa kwamba tunayowaambieni ni Kweli.

193 Sasa kukujua wewe, unajua sikujui. Hiyo ni, inua mkono wako kusudi watu waone ya kwamba wewe . . . Mimi, mimi sijapata kumwona mtu huyu maishani mwangu. Yeye ni mwanamume tu anayesimama hapa. Mwulizeni yeyote wa hao wengine. Lakini unaugua henia. Pia una bawasiri. Hiyo ni kweli. Umetoka mbali, kufika hapa. Hata wewe si Mmarekani. Wewe ni Mkanada. Ulimleta na mwanao ambaye ana matatizo ya bongo. Hiyo ni kweli. Unataka nikwambie unakotoka? Umetoka mkoa wa Sasketchewan, jiji la Saskatoon. Amini kwa moyo wako wote, Naye Mungu atakurudisha nyumbani ukiwa mzima, pamoja na mwanao, kama ukiamini. Unaamini? Mungu akubariki.

194 Mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Bwana Mungu angali anabaki ni Mungu. Mnaona? Hakuna mwingine ila Yeye.

195 U hali gani? Huyu hapa mama, mgeni kwangu, labda ana umri mkubwa zaidi kidogo. Sijapata kumwona; bali yeye ni—yeye ni mwanamke tu anayesimama hapa. Itanibidi kuharakisha, maana nina dakika saba ama nane tu sasa, mnaona. Angalia tu hapa. Je! unaamini ya kwamba mambo haya ni kweli? Kwa moyo wako wote? Unajua haiwezekani mimi

kujua shida yako, wala chochote kukuhusu wewe. Bali si jambo lisilowezekana kwa Mungu kujua, kwa kuwa Yeye alijua hata kabla ulimwengu usijakuwapo. Hiyo si ni kweli? [Dada huyo anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.]

196 Ni wangapi wanaoamini hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika. Yeye alijua kila wakati ungepepesa jicho lako. Yeye hana kikomo. Na hebu wazia tu; kwa neema Yake ametupa, kwa Injili Yake, jambo lile lile aliloahidi kufanya. Basi pana Mbingu, nasi tunaelekea huko. Nasi tuko katika Waefeso hii sasa hivi. Tuko kwenye hii, tunatoka kwenye moja, tukaingia nyingine.

197 Una shida nyingi sana, matatizo, shida chungu nzima. Nawe hutoki hapa. Umetoka magharibi mwa hapa. Umetoka Kalifornia. Hiyo ni kweli. Pia una mwana anayeteseka. Hiyo ni kweli. Wewe. . . Kuna jambo fulani, ninaendelea kuona maji ama ziwa kubwa mno. Loo, ni, una—una mtu aliye karibu nawe, anayeishi Chikago, anayenijua mimi. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Sasa, unajua sikujui mimi, bali unaamini Mungu anajua wewe ni nani? Bibi McGuire. Umepata ombi lako. Nenda nyumbani ukimshukuru Mungu.

U hali gani? Wewe ni kijana mashuhuri.

198 Bali maradhi na magonjwa hayana upendeleo. Ni wangapi wanaojua hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Tunajua tu hayana upendeleo.

199 "Kama unaweza kuamini kwa moyo wako wote na nafsi yako yote!" Hiyo pumu ingekuacha kama ungeamini kwa moyo wako wote.

200 Shida ya kifua, unaamini ingekuacha, pia, dada, nawe ungepata afya? Uligusa nini? Yuko futi ishirini kutoka kwangu, ama zaidi. Alimgusa Bwana. Ni msongamano, wa neva. Utapata afya.

201 Hili ni jambo zuri lililomfanya msichana huyu kusimama hapa. Ni mgeni kabisa. Sijapata kumwona mwanamke huyu. Bali ameletwa hapa na mtu mwingine. Na kilichomleta hapa, ni kwa sababu alisikia kanda niliyoitengeneza. Naye yupo hapa akiutafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hilo ndilo lililomleta hapa hasa. Hiyo ni kweli, ewe msichana. Hiyo ni kweli. Njoo hapa.

202 Mungu mpendwa, jalia mtoto huyu anayesimama hapa, ambaye anatoka gizani kuingia kwenye Nuru, jalia ampokee Roho Mtakatifu; aende nyumbani mwake na kwa wapendwa wake, akawaonyeshe mambo makuu ambayo Yesu amemtendea. Amina.

Mungu akubariki. Usitie shaka. Amini.

203 Mungu anaweza kuponya wasiwasi wa kila namna na (unaamini hilo?) ugonjwa wa pumu, na kukupa afya. Unaamini

hilo? Basi nenda zako, amini kwa moyo wako wote. Mungu na akubariki, ndugu.

204 Una umri gani? [Dada anasema, “Thelathini na minane.”—Mh.] Huna budi kutoka kwenye wasiwasi huo kabla muda haujaenda sana, sivyo? Una hali za kuishiwa nguvu za kila namna, na una matatizo ya kila namna. Bali yamekuacha sasa. Naam, bwana.

205 Mungu huponya wasiwasi, ugonjwa wa tumbo, pia. Unaamini hilo? Basi nenda ukale chochote utakacho. Yesu Kristo alikuponya.

206 Mnaamini huko nje, kila mmoja wenu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

207 Yupo mtu anayeketi amevaa sha—shati, akiniangalia, naam, aliinama akaliangalia shati lake papo hapo. Naam. Unaamini Mungu anaweza kuponya ugonjwa wa tezi, anaweza kukupa afya? Ulikuwa ukiamini wakati huo (sivyo?), wakati ule ule maskini mvulana huyu alipoponywa ugonjwa huo wa pumu. Nenda nyumbani, mpenzi, utapata afya, pia, unaona. Amini kwa moyo wako wote.

208 Maskini mama huyo anayeketi karibu na mke wako hapo, ungeweza kuamini macho yako yatapona, pia? Unaamini ya kwamba Mungu ataponya ugonjwa huo wa jicho? Inua mkono wako kama hilo ndilo ulilokuwa ukiombea. Unaona?

Waligusa nini? Yesu Kristo Mwana wa Mungu.

209 Unaamini? Unaamini, ewe kijana mwanamume? Mungu anaweza kuponya ugonjwa huo wa damu, akupe afya, (utaamini hilo?) akuondolee kisukari hicho na kukuponya. Unaamini hilo? Nenda ukamwambie unaamini, na uondoke.

210 Njoo, bwana. Una ugonjwa wa tumbo. Unaamini Mungu anaweza kuuponya, upate afya? [Ndugu huyo anasema, “Naam, ninaamini.”—Mh.] Nenda, uamini; utapata afya, na kuponywa.

211 Njoo, mlete maskini mvulana huyu. Angalia hapa, mwanangu. Umetoka mbali. Wakati mwingine mabadiliko katika usawa wa bahari, mabadiliko ya hali ya hewa, yatafanya hivyo, kuuponya ugonjwa wa pumu. Ila kuna uponyaji mmoja wa hakika, Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Yeye alimtoa Mwanawe, ili wako apate kuponywa. Unaamini hilo? Amini kwa moyo wako wote, nao utakuacha. Atakuwa mzima, mtu mwenye afya. Mungu akubariki, dada.

212 Unaamini? Je! Mungu angali anafanya vitendawili? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yasiyoelezeka, yasiyowazika, mambo ambayo watu wasingeelewa jinsi yangekuwa, bali yangali ni kweli, sivyo? [“Amina.”] Sasa ni wangapi wanaohisi, na kujua rohoni mwako, ya kwamba hapana budi kuweko na kitu Fulani hapa ambacho kimepita ufahamu wa mwanadamu?

213 Sasa, nafikiri tuliita angalau watu kumi na watano kwenye mstari huo, kila mmoja wao; na wanne ama watano, sita, pale mstarini, wasio na kadi za maombi, ama vyovyote walivyokuwa pale mstarini, huko kwenye wasikilizaji pale. Lakini tuko sasa hivi na dakika moja tu ya wakati, wa kufunga.

214 Je! Yeye alifanya jinsi hasa alivyosema atafanya? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa ni wangapi wanaoamini ni yeye yule jana, leo, na hata milele, wanaouhisi Uwepo Wake? ["Amina."] Sasa mmeuona Uwepo Wake. Sasa jicho lako limeona, masikio yenu yamefahamu, Naye Mungu amethibitisha, mbele ya macho yenu, Uwepo Wake. Na huo ndio unaouhisi wakati wote, unaokuhukumu wakati umekosea, na kukwambia usifanye hivyo, Mungu yuyo huyo ameweza kuonekana kwenu hapa alasiri ya leo, katika matendo Yake. Ni wangapi wanaosema "amina" kwa jambo hilo? ["Amina."] Hakika, ndivyo ilivyo. Sasa Yeye yupo hapa.

215 Je! kuna mtu hapa miongoni mwetu, ambaye hajawahi kuwa Mkristo; hajawahi kukiri, kamwe hujapata kwenda kanisani? Waweza kusimama, na kusema, "Ninataka kusimama, si kwako, ewe mhudumu; bali nataka kusimama wakati nikiwa Mbele ya Mtu huyu, Yesu Kristo, ambaye ni Roho Mtakatifu juu yetu sasa. Nataka kusimama na kusema, 'Ninataka uniokoe na dhambi zangu'"? Hivyo tu ndivyo ninavyokutaka ufanye, simama tu, na hilo litashuhudia. Hilo ndilo tu tulilo na wakati wa kulifanya. Sema, "Nataka kuwa Mkristo." Simama kwa miguu yako, kisha uketi moja kwa moja.

216 Kuna mmoja jengoni? Ni wangapi waliomo humu jengoni? Sipaswi kusema, "Kuna mmoja?" maana huenda kukawa na zaidi ya mmoja. Ni wangapi humu jengoni watasimama sasa hivi, na kusema, "Nimekuwa makosani, Mungu. Nisamehe. Nitasimama kukupa ushuhuda ya kwamba nimekuwa makosani. Nitaketi chini wakati nikiwa hapa Mbele Zako. Nitaketi chini"? Simama tu.

217 Kuna mmoja, kuna zaidi ya mmoja? Mkono mmoja. Mungu akubariki, kijana mwanamume. Kuna mwingine? Mungu akubariki. Kuna mwingine? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, ndugu. Kunaye? Mungu akubariki, huko nyuma. Kuna mwingine, "Nimekuwa makosani. Mungu, nisamehe"? Mungu akubariki, bwana. "Nimekuwa makosani. Na—nasikitika, Bwana." Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki.

218 Kumekuwako na mtu yeyote ambaye ameitilia shaka huduma hii, na umeshawishika sasa kwamba ni ya kweli? Simama hapo, na useme, "Mungu, nisamehe." Inua tu mkono wako, useme, "Ki—kidogo nilitilia shaka, Ndugu Branham; yote yamekwisha sasa." Inua mkono wako. Hamna hata mmoja? Asanteni.

219 Ni wangapi wanaoamini jambo Hili? Isingeweza kuwa ni mimi; bali ni Kristo, Mwana wa Mungu. Asanteni. Basi mtaona mambo makuu kuliko haya yakifanywa, mradi tu mtaamini. Dumuni tu pamoja na Kristo. Nitafanya niwezayo kudumu pamoja Naye, mimi mwenyewe.

220 Sasa ni wangapi hapa walio wagonjwa na wahitaji, inua mkono wako, "Mimi—mimi ni mgonjwa, Ndugu Branham, ni mhitaji"? Mnaona, hebu waangalieni hao watu. Sasa je! mtafanya jambo hili na kuamini tu neno langu kiasi hiki? Hebu tuwekeane mikono mmoja kwa mwingine, wakati nikiinyosha mikono yangu kuwaelekea.

Na tuombe.

221 Mungu mpendwa, ninakuletea maskini wasikilizaji hawa, alasiri ya leo, ambapo tumesikia na kulisoma Neno la Mungu. Tunajua ya kwamba kila sehemu yake ni Kweli, kwa kuwa ni Neno Lako. Sio sasa tu hivi tunaamini kwamba ni la kweli; tunajua ni la kweli. Tumekuona, Bwana, ukifanya jambo ambalo litawafanya watu wajue ya kwamba kungali. . .Mbali na kitendawili cha—cha ulimwengu, na anga, na kanuni za kawaida za Mungu, tunaweza kuona hapa ambapo kanuni za mauti zinafanya kazi katika mwili wa mwanadamu, ambapo sayansi imeshindwa ku—kuponya kwa utafiti wao. Na, Bwana, tunashukuru kwa ajili ya watu hao. Kamwe hatuwadharau. Tunashukuru kwa ajili yao. Lakini, Bwana, inapofikia mahali ambapo hawawezi kufanya la zaidi, sasa tunauona mkono Wako mkuu ukiingia; tukijua ya kwamba hakuna mtu angeweza kuwaponya, kwa kuwa angekuwa ni daktari, ama imbidi kuchukua tiba fulani. Bali kumwona Mwana wa Mungu akishuka, na ambaye aliifanya ahadi, ambayo sote tunaiamini.

222 Na kila mtu aliuinua mkono wao juu, ambao hawakuwa wameokoka, na—na walitaka kuokoka. Mungu, kitu fulani kiliuonya moyo wao. Baadhi yao walisema walikuwa "makosani," labda walirudi nyuma na walitaka kurejea. Ninaomba ya kwamba utamrudisha kila mmoja. Kwa maana wanajua, Bwana, na walijua. . .Huenda wengi wao walinijua, ama wamenisikia, miaka hii, na wanajua ya kwamba hakuna jambo jema katika mwanadamu, na hasa mimi. Kungewezaje kuwako na jambo lolote zuri? Lakini hata hivyo waliliona hilo Neno, ambalo Mungu aliahidi, likidhihirishwa. Wameshawishika kwamba ni Kweli. Wamelikubali.

223 Wengi hapa nisingeweza kuwaleta jukwaani. Na, Baba, Wewe unanishuhudia, kamwe sijapata kusema ya kwamba lingekuwa ni jambo ambalo ningeweza kufanya, si zaidi ya kujitolea mwenyewe Kwako, na kukuacha Wewe uniondoe njiani na kuiweka Roho Yako mle ndani ikatende kazi. Sasa, Baba, tukiona kuwa mtu mmoja anaweza kufanya jambo hilo, mwingine anaweza kufanya, ninaomba ya kwamba kila mtu

aliyeweka mkono wake juu ya mwingine, aliye mgonjwa na anayeteseka, ataponywa wakati uu huu.

224 Jalia Roho Mtakatifu aliye mkuu apitie humu jengoni sasa hivi na kumponya kila mtu. Mwokoe kila mtu, Bwana. Tupe tukio kuu. Mimina Roho Mtakatifu, Bwana, juu ya wasikilizaji hawa. Loo, tunakutazamia Wewe kufanya mambo makuu juma hili lijalo. Na iwe hivyo tu, Bwana, sasa hivi, katika Jina la Yesu Kristo.

225 Sasa hebu sote na tusimame kwa miguu yetu. Unaamini kwa moyo wako wote? Sasa sijui kama dada yetu, kwenye piano pale, angetupa sa—sa—sauti kidogo ya huu, "Nitamsifu. Nitamsifu." Mmeusikia huo? Sasa hebu na tuuimbe, pamoja. Sasa tutatumaini kukutana nanyi kesho jioni. Sasa tutafumukana rasmi, katika dakika moja, bali nataka kuimba wimbo huu pamoja nanyi. Vema, haya twende.

> Nitamsifu, (na tuinue mikono yetu) nitamsifu,
> Msifuni Mwana-kondoo aliyechinjwa kwa ajili
> ya wenye dhambi;
> Mpeni utukufu, enyi watu wote,
> Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila waa.

226 Na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi ya kufumukana. Vema, Ndugu Jewel Rose atatururuhusu tufumukane. Mungu akubariki, Ndugu Rose, tunaponinii . . .

Kitendawili SWA65-0117
(A Paradox)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili alasiri, tarehe 17 Januari, 1965, kwa ajili ya kiamshakinywa cha Ushirika wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Hoteli ya Westward Ho huko Phoenix, Arizona, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org